UKURASA WA 3
**Mwinyi** aahidi fidia waliopisha miradi ujenzi wa bandari, barabara



UKURASA WA 4
**Wajawazito** wajifungua kwa kutumia tochi ya simu




# Nipashe

Jumamosi Novemba 25, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581505

www.ippmedia.com



0745 700710 LIKE & FOLLOW US

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com




**WAN-BISSAKA ATAKIWA DR CONGO**

UKURASA 22



DCI RAMADHAN KINGAI

# Mke wa ofisa polisi auawa na mchepuko


• **Chanzo** chaelezwa ugomvi wa mtoto, naye ajiua kwa kujichana na kisu... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza kwenye Mkutano wa 23 wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) katika viwanja vya Hoteli ya Ngurdoto, Arusha jana. **PICHA: IKULU**

## Samia ataka kuondolewa vikwazo visivyo vya forodha EAC

UKURASA 2



## Watumishi afya lazima kupimwa homa ya ini

UKURASA 3

**MICHEZO** **AZIZ KI AENDELEA 'KUKIMBIZA' LIGI BARA** UK.24 **KATUNI** UK.6

## Bibi auawa mbele ya wajukuu madai imani za kishirikina

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MKAZI wa Kijiji cha Chombe, wilayani Sumbawanga mkoani Rukwa, Mwashi Salita (60), ameuawa mbele ya wajukuu zake kwa kukatwa mapanga kutokana na imani za kishirikina.

Tukio hilo lilitokea Novemba 20, mwaka huu, saa 1:00 usiku, baada ya watu wasiojulikana kuvamia nyumbani kwake kisha kumkata mapanga na kukimbia.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Kamishna Msaidizi (ACP) Shadrack Masija, alisema jana kuwa watu hao walikwenda nyumbani kwa mwanamke huyo wakiwa na silaha mbalimbali za jadi.

Hata hivyo, Kamanda Masija alisema watu watatu wanaotuhumiwa kuhusika na tukio hilo, wamekamatwa na watafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

Kamanda Masija alisema walipofika nyumbani kwa bibi huyo, walimkuta akiwa na wajukuu zake ndipo walipomvamia na kumpiga.

"Kabla ya watuhumiwa hao kumkata mapanga, walimpiga kichwani kwa kutumia kitu butu, kitendo kilichosababisha kuanguka chini na kushindwa kupata msaada kwa kuwa alikuwa yupo na watoto.

"Walimkata mapanga sehemu mbalimbali za mwili na kumsababishia majeraha makubwa yaliyovuja damu nyingi. Hakupata msaada wowote, hivyo kusababisha kifo chake muda mfupi baadaye," alisema.

Kamanda huyo alisema kuwa baada ya polisi kuanza uchunguzi wa tukio hilo walifanikiwa kuwakamata watu watatu wanao tuhumiwa kuhusika na tukio hilo.



Dereva wa boda-boda akiwa amewabeba wanafunzi watatu kwenye pikipiki yake katika eneo la Goba Tegeta A, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam hivi karibuni, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mke wa ofisa polisi auawa na mchepuko

**Na Mwandishi Wetu**

MWANAMKE mmoja ambaye ni mke wa ofisa wa polisi, ameuawa na mtu ambaye anadaiwa kuwa mpenzi wake, chanzo kikitajwa kuwa ugomvi wa mtoto anayedaiwa kuwa amezaa naye.

Mwamume huyo ambaye umri wake anadaiwa kuwa ni kijana, aliingia katika makazi ya polisi, Mbweni, Kinondoni mkoani Dar es Salaam na kusababisha mauaji hayo, kisha naye kujiua.

Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (ZCO) wa Jeshi la Polisi Kanda Maalamu ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi (ACP) Faustine Mafwele, alithibitisha jana kutokea kwa tukio hilo.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake, ACP Mafwele alisema tukio hilo lilitokea Novemba 20, mwaka huu (Jumatatu wiki hii) huku akisema chanzo chake bado hakijafahamika.

"Bado tunaendelea na upelelezi na kwa bahati mbaya sana wamefariki (dunia) wote ambao wangeweza kueleza kiini cha tatizo," alisema huku akibainisha kuwa bado wanafuatilia historia ya kijana huyo ili kujua vizuri chanzo cha kutekeleza mauaji hayo.

ACP Mafwele alisema mwanamke huyo ambaye ni mke wa askari ameacha mtoto mwenye mwaka mmoja na miezi mitano.

"Yule mtoto alikuwa anaokolewa na mama yake si kwamba alirushwa nje kama inavyoelezwa," alisema.

Hata hivyo, mashuhuda waliiambia Nipashe kwamba tukio hilo limewashtua kwa kuwa kijana amevamia makazi ya askari na kufanya mauaji.

Shuhuda mmoja (jina linahifadhiwa) alisema chanzo cha mzozo huo ni uhusiano wa kimapenzi kati ya mke wa askari na kijana aliyedaiwa kusababisha mauaji.

"Tunavyosikia ni kwamba huyu kijana alikuwa ana uhusiano wa kimapenzi na huyu mke wa askari (jina linahifadhiwa) na kwamba walizaa huyo mtoto lakini inaonekana baadaye walitofautiana," alisema shuhuda huyo.

Alisema kijana huyo aliamua kwenda nyumbani kwa mwanamke huyo kudai mtoto wake ndipo ulipotokea mzozo baina yao uliosababisha vifo.

"Kulikuwa na mzozo kwa muda kidogo ndipo tukaona mtoto akirushwa kupitia dirishani kwenye ghorofa katika nyumba aliyokuwa akiishi mwanamke na mume wake. Watu walimwokoa mtoto na kwa bahati mbaya mama yake alichomwa kisu na akaanguka chini pia," alisema.

Taarifa zaidi zinasema baada ya kumchoma kisu mwanamke huyo, kijana huyo naye alijichoma kisu na kusababisha kupata majeraha makubwa na hatimaye kufariki dunia.

ACP Mafwele alisema mwanamke huyo pamoja na kijana aliyesababisha tukio walifariki dunia wakati wanapelekwa hospitalini.

# Rais Samia ataka kuondolewa vikwazo visivyo forodha EAC

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameelekeza mawaziri na watendaji masuala ya biashara na forodha, kukutana na kumaliza vikwazo vyote visivyo vya kiforodha katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Wakati Rais Samia akielekeza hayo, Katibu Mkuu wa EAC, Dk. Peter Mathuki, amesema Mkutano Mkuu wa 23 wa Wakuu wa Nchi za EAC, umeazimia kuwa ifikapo Juni 14, 2024, nchi tano wanachama ambazo hazijakamilisha mapendekezo ya kuanzishwa shirikisho la kisiasa, kukamilisha ukusanyaji maoni ya wananchi. Nchi zilizokamilisha mapendekezo ya kukusanya maoni ya wananchi kuhusu shirikisho la kisiasa mpaka sasa ni Burundi, Rwanda na Kenya.

Aidha, wakuu hao wa nchi, wameridhia ombi la Somalia la kuwa mwanachama wa Jumuiya hiyo kuanzia Novemba 24, mwaka huu. Somalia inakuwa nchi ya nane EAC, ikiungana na Kenya, Tanzania, Uganda, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Sudan Kusini. Somalia iliwasilisha ombi la kujiunga na Jumuiya hiyo mwaka mmoja uliopita.

Baada ya Somalia kutangazwa kuwa mwanachama mpya wa EAC, Rais wa Somalia, Hassan Sheikh Mahamud, alisema wananchi wake wana furaha kubwa kuona wakuu wa nchi za Afrika ya Mashariki, wamekubali ombi lao kuwa sehemu ya familia moja ya EAC.

"Somalia tutakuwa tayari kutekeleza sera zote, tutalipa michango yote ya jumuiya na tutashiriki kila hatua au matakwa ya uanzishaji wa EAC. Tunaona fahari kuwa sehemu ya jumuiya ya EAC, kwa sababu ni familia moja na mfano wa kuigwa katika ukanda wa Afrika," alisema. Katika mkutano huo, Rais wa Burundi, Evariste Ndayishimiye, alikabidhi kijiti cha Uenyekiti wa EAC, kwa Rais wa Sudan Kusini, Salva Kiir.

Akifafanua zaidi kuhusu vikwazo visivyo vya kiforodha, Rais Samia, alisema wananchi wa Afrika Mashariki, wanataka kufanya biashara kwenye mazingira rafiki na si vikwazo.

"Nchi za Afrika Mashariki zina mambo mengi ya kufanana kuliko ya kutofautiana, hivyo ni wakati sasa vikwazo hivyo viondolewe ili kuruhusu biashara baina ya nchi wanachama," alisema.

Mkutano huo wa wakuu wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), pamoja na mambo mengine ulijadili kuhusu masuala ya tabianchi na usalama wa chakula.

Vilevile, lilikuwamo suala la usalama Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na ombi la Somalia, kujiunga na jumuiya hiyo. Rais wa Kenya, William Rutto, alisema ni lazima sasa nchi wanachama wa EAC zisikubali kupoteza fursa zilizoko katika nchi wanachama kwa kuwa zimejaliwa utajiri wa rasilimali nyingi ikiwamo ardhi.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE**

HALMASHAURI YA WILAYA KOROGWE

25/11/2023

**TANGAZO LA MNADA**

Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe inawatangazia wananchi wote kuwa tarehe 08/12/2023 itauza kwa njia ya Mnada wa hadhara vifaa vifuatavyo:-

| Na | Aina ya kifaa | Idadi | Hali ya kifaa |
|---|---|---|---|
| 1 | Magari | 4 | Hayatembei |
| 2 | Pikipiki | 3 | hazitembei |

**MASHARTI YA MNADA WA MAGARI NA PIKIPIKI**

1. Magari na pikipiki zitauzwa kama zilivyo na mahali yalipo.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa hapohapo amana (deposit) isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) kwa magari na pikipiki. Malipo yote ya magari na pikipiki yakamilike katika muda wa siku kumi na nne(14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa kifaa husika na amana aliyolipa haitarejeshwa.
3. Mnunuzi atatakiwa kuondoa /kuchukua kifaa alichonunua katika muda wa siku saba(07) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
4. Ruhusa ya kuangalia magari/pikipiki itatolewa siku mbili (2) kabla ya tarehe ya mnada kuanzia 3:00 asubuhi mpaka saa 10:00 jioni katika ofisi ya halmashauri ya wilaya jengo la zamani mkabala na kituo cha Polisi Korogwe.
5. Mnada utafanyika siku ya Ijumaa tarehe 08/12/2023 muda ni kuanzia saa 04:00 asubuhi, mahali ni jengo la zamani la halmashauri ya wilaya Korogwe .

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
S.L.P 584
KOROGWE

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
P.O.Box 584
KOROGWE

## HABARI KITAIFA

# Watumishi afya lazima kupimwa homa ya ini

**Na Restuta James**

SERIKALI imeongeza nguvu katika vita dhidi ya homa ya ini (Hepatitis B), magonjwa ya ngono na ukimwi, huku watumishi wa afya wakitakiwa kuchoma chanjo ya ugonjwa huo.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, aliyasema hayo jijini Dar es Salaam jana alipokuwa akizindua Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi, Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini (NASHCOP).

Alisema lengo la mpango huo ni kuwezesha wadau wanaopambana na ukimwi kugusa pia magonjwa ya ngono kwa kuwa yanaambatana katika maambukizi.

Waziri Ummy alisema takwimu zinaonesha kuwa kuanzia Januari hadi Septemba mwaka huu, watu 6,542 waliokwenda hospitali walibainika kuwa na magonjwa ya ngono yakiwamo kisonono na kaswende pamoja na virusi vya Ukimwi (VVU).

"Huu ni mpango jumuishi wa kukabiliana na magonjwa ya ngono, Ukimwi na homa ya ini niwaombe tujikite katika magonjwa ya ngono kama kaswende na kisonono kwa sababu yapo katika kiwango cha juu cha maambukizi hasa kwa makundi maalumu kama wanaojidunga dawa za kulevya," alisema.

Ummy alisema kampeni ya kuyakabili ni pamoja na kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Alifafanua kuwa mpango unalenga kuhamasisha kinga, udhibiti na tiba na kwamba kuunganisha homa ya ini kwenye mkakati ni kuelimisha jamii umuhimu wa chanjo ya ugonjwa huo.

"Chanjo ya homa ya ini ni kwa ajili ya kujikinga maisha yako yote kwa sababu ukipata maambukizi gharama za matibabu ni kubwa sana.

"Tumefanikiwa kuwafikia watumishi wa afya 23,000 ambao wamepata chanjo ya homa ya ini lakini jumla wapo zaidi ya 110,000 hapa nchini wajikinge wenyewe kabla hawajaanza kuwakinga wengine. Na hapa nitoe maelekezo kabisa, watumishi wa afya ni lazima wachanje," alisema.

"Lazima iwe ni lazima kwa sababu haiwezekani mtu anakwenda hospitali kwa tatizo la jino anarudi na homa ya ini si sawa. Tunaamini kupitia mpango huu tutawafikia watumishi wa afya, makundi maalumu na wote waliopo kwenye hatari ya kupata maambukizi kama uhamiaji na wote wanaohudumia wananchi wengi," aliongeza.

Pia aliwataka wananchi kupata chanjo hiyo, kuzingatia ulaji unaofaa pamoja na kufanya mazoezi kila siku.

Kuhusu magonjwa ya ngono, Waziri Ummy alishauri jamii kujenga utamaduni wa kupima na kupewa matibabu sahihi kulingana na ugonjwa badala ya kujinunulia dawa.

"Tusipopambana kudhibiti matumizi holela ya dawa tutapata magonjwa yasiyo na tiba hebu mpango huu tuweke mkazo kwenye elimu ya matumizi sahihi ya dawa," alisema.

Baadhi ya wadau walioshiriki uzinduzi wa NASHCOP waliishauri serikali iongeze vifaa tiba, dawa na watumishi kwenye zahanati na vituo vya afya ili wananchi wapate huduma kwa urahisi.

# Mwinyi aahidi fidia waliopisha miradi ujenzi bandari, barabara

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imeahidi kuwalipa fidia ya vipando (Vesper) na majengo wananchi wote wa eneo la Bumbwini waliopitiwa na mradi wa barabara na ujenzi wa bandari jumuishi ya Mangapwani.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyasema hayo jana alipozungumza na wananchi wa Bumbwini Misufini, shehia ya Kidanzini, kijiji cha Mwembe Mdema, Mkoa wa Kaskazini Unguja, alipofanya ziara kukagua ujenzi wa nyumba za fidia kwa wananchi waliopisha miradi ya maendeleo kijijini hapo.

Alisema tayari ulipwaji wa fidia kwa baadhi ya wananchi hao umeanza kwa wakaazi wa Mangapwani na baadaye kumalizia vijiji vingine vilivyopitiwa na miradi hiyo.

"Kwa wale wote wanaostahili kulipwa fidia, iwe ya vipando au majengo, tunahakikisha fidia zenu mtalipwa nyote kwa kipidi kifupi," alisema Dk. Mwinyi.

Aidha, Rais Dk. Mwinyi aliwashauri viongozi wa jimbo hilo, kushirikiana na mkandarasi wa mradi wa nyumba za wananchi zinazoendelea kujengwa kwenye maeneo ya Mwembe Mdema, Shehia ya Kidanzini na nyumba za Mangapwani kwa kuangalia mahitaji halisi ya aina ya nyumba wananchi watakazoridhika nazo.

Pia aliishauri kamati inayosimamia ujenzi wa nyumba hizo, kushirikiana na mkandarasi kujenga nyumba zitakazokidhi haja za walengwa ili kuwaepushia usumbufu wa baadae.

Waziri wa Ujenzi na Mawasiliano, Dk. Khalid Salum Muhamed, alisema hatua za ujenzi wa awali wa nyumba hizo zitasaidia kuboresha mwendelezo wa nyumba zitakazofuata kwa kuepuka changamoto zilizojitokeza baada ya kukamilika nyumba mbili za mwanzo.

Dk. Khalid pia alisema mbali na fidia za mazao na nyumba, wananchi waliopoteza maeneo yao, vikiwamo viwanja, tayari serikali imeunda kamati inayojumuisha wataalamu wa ardhi na wanasheria ili kukamilisha ahadi ya serikali ya kulipwa na kwamba tayari eneo hilo limefanyiwa tathmini na ripoti imetoka.

Kampuni ya Orkun kutoka Uturuki, inayojenga nyumba hizo, imeahidi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufanya maboresho kwa mujibu ya maelekezo wanayokubaliana.

Ujenzi huo unatarajiwa kukamilisha nyumba 370 kwa wananchi wa maeneo ya Bumbwini Misufini pamoja na wakaazi wa maeneo ya Mangapwani ikiwa ni sehemu ya fidia yao watakayopewa na serikali baada ya kupisha miradi ya maendeleo iliwemo miundombinu ya barabara na ujenzi wa bandari kubwa ya Mangapwani.

# TANGAZO/ NOTISI YA MNADA WA HADHARA

**LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD; HEDANE ENTERPRISES (T) LIMITED; HARVESTER CAPITAL INVESTMENT; MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD na KOTI BROTHERS COMPANY LIMITED** kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED,** tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama ilivyo onyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya Siku Kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya Notisi /Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | OSCAR BONIFACE KAZIULAYA | OSCAR BONIFACE KAZIULAYA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI Na.84432, PLOT Na.1308, BLOCK 'D' | MTONI KIJICHI, MANISPAA YA TEMEKE, DAR ES SALAAM | 11/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |
| 2 | MCHONVU COMPANY LIMITED | ZUBERI JUMA MCHONVU | KIWANJA CHENYE HATIMILIKI Na.36489, PLOT Na.526, BLOCK 'G' | SAME, KILIMANJARO | 11/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | HEDANE ENTERPRISES (T) LIMITED |
| 3 | MCHONVU COMPANY LIMITED | ZUBERI MOHAMED MCHONVU | NYUMBA YENYE HATI MILIKI Na.43465, PLOT Na.87, BLOCK 'H' | MAHUU, WILAYA YA SAME, MKOA WA KILIMANJARO | 12/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | HEDANE ENTERPRISES (T) LIMITED |
| 4 | MCHONVU COMPANY LIMITED | MOHAMED JUMA MGHANGA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI Na.SAM00047, ARDHI Na.SAM/STA/SHB/30 | KILUNGULE 'A', KIMARA, MANISPAA YA KINONDONI | 13/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | HEDANE ENTERPRISES (T) LIMITED |
| 5 | WAIDA MARCO MANO | MAULID JUMA NJIKU | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | BURKA, OLASITI IN ARUSHA MUNICIPALITY | 12/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | HARVESTER CAPITAL INVESTMENT |
| 6 | SALOME NELSON KIBONA | FELIX LEORNARD MWANGU | KIWANJA CHENYE HATI YA MAUZIANO Na.11, Kitalu "E" | IYUMBU NORTH, DODOMA CITY | 11/12/2023, SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | KOTI BROTHERS COMPANY LIMITED |
| 7 | SOSPETER JOSEPH APOLINARY | JULIANA APOLINARY OLOTU | NYUMBA YENYE HATI MILIKI Na.65689, PLOT Na.1049, BLOCK "KKK" | SHIRIMATUNDA, MANISPAA YA MOSHI MJINI | 14/12/2023 NAKUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD |
| 8 | WINIFRIDA J MUSHI | EDINGTON MELKIDEZECK NYELLA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | MTAA WA MSUFINI, KATA YA MSARANGA WILAYA YA MOSHI | 15/12/2023 NAKUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD |
| 9 | YONA MARTIN MJEMA | YONA MARTIN MJEMA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | MTAA WA KIVULINI, KILEO WILAYA YA MWANGA | 16/12/2023 NAKUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD |
| 10 | SPRIAN GEORGE CHUWA | SPRIAN GEORGE CHUWA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | MTAA WA MJI MPYA, KATA YA MABOGINI WILAYA YA MOSHI | 18/12/2023 NAKUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD |
| 11 | JOEL SILVESTA SIMBI | JOSEPHINE HASHIMU CHOMBO | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | MTAA WA MIEMBENI, LANGONI, WILAYA YA MOSHI | 19/12/2023 NAKUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindii wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyopungua 25% ya bei iliyofikiwa siku yamnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

| LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD | HEDANE ENTERPRISES (T) LIMITED | HARVESTER CAPITAL INVESTMENT | KOTI BROTHERS COMPANY LIMITED | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD |
|---|---|---|---|---|
| P.O.Box 68172 | P.O.Box 1211 | P.o.Box 11898 | P.O. Box 5022 | P.O.Box 12943 |
| Dar es Salaam, Tanzania | Arusha, Tanzania | ARUSHA | Dar es Salaam | Arusha, Tanzania |
| Tel: 0620 848 565/ 0714 598 559 | Tel: 0735 277 331/ 0759 648 448 | Tel: 0784 200283/ 0767529605 | Tel: 0757 785 247/ 0677 070 958 | Tel: 0752 632 033/ 0628512033 |
| Email: lehalelglc@gmail.com | Email: philbertmussali@gmail.com | Email: harvestercapital558@gmail.com | Email: kotibrotherstz@gmail.com | Email: mangwembe@gmail.com |

# Makada 83 warejesha fomu kumrithi Zelothe

**Godfrey Mushi,** ARUSHA

MAKADA 83 kati ya 88 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) waliojitokeza kuomba kuteuliwa kugombea kujaza nafasi ya Mwenyekiti wa CCM, Mkoa wa Arusha, wamerejesha fomu hizo, baada ya kufungwa rasmi kwa pazia hilo jana.

Mchakato huo unafanyika kujaza nafasi iliyoachwa wazi na Zelothe Steven, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) wa Jeshi la Polisi nchini ambaye alifariki dunia Oktoba 26, mwaka huu, akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Mzena, Dar es Salaam.

Akitangaza kufungwa pazia hilo juzi, Katibu wa CCM Mkoa wa Arusha, Mussa Matoroka, alisema wanachama watano walishindwa kutimiza vigezo vya mchakati huo.

Aidha, Matoroka alionya makada waliochukua fomu hizo kuacha kujipitisha kabla ya wakati kufanya kampeni za siri ili kutengeneza mazingira ya ushawishi na kukubalika kwao.

Alisema pazia la uchukuaji wa fomu za kujaza nafasi hiyo, lilianza Novemba 21 na kufungwa Novemba 23, mwaka huu.

"CCM ina intelejensia kubwa, na hivi sasa inaendelea kufuatilia mienendo yote ya wagombea wanaochukua fomu, na ikithibitika kuwa kuna mgombea anafanya kampeni kwa namna yoyote ile, hatua kali za kikanuni zitachukuliwa dhidi yake ikiwa ni pamoja na kuengua jina lake.

"Marufuku kwa wagombea wote wanaochukua fomu kuanza kufanya kampeni za kuomba kura na kufanya kampeni za kuwapaka matope wagombea wenzao, kwa wajumbe wanaotakiwa kupiga kura.

"Hiyo ni kwa sababu, bado ni mapema mno na watambue kwamba tunawafuatilia kwa karibu na ikithibitika kuwa kuna wagombea wameanza kufanya kampeni majina yao yataenguliwa mara moja," alisema.




Mkurugenzi wa MISA–TAN, Elizabeth Riziki akizungumza wakati akifungua mkutano wa kuimarisha usawa wa kijinsia na uhuru wa vyombo vya habari, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajawazito wajifungua kwa tochi ya simu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAJAWAZITO takribani 100 kila mwezi hujifungua kwa kutumia tochi ya simu katika zahanati ya kijiji cha Kiganila, Kata ya Selembala, wilayani Morogoro baada umeme wa jua uliokuwa ukitumika, mtambo wake kuharibika tangu 2021.

Akizungumza katika mkutano wa Baraza la Madiwani kupitia taarifa za kata za robo ya kwanza kwa mwaka wa fedha 2023/24, Diwani wa Selembala, Msafiri Gilla, alisema wajawazito hao hujifungua kwa tochi kutokana na zahanati hiyo kukosa huduma ya umeme.

Alisema zahanati hiyo iliyojengwa mwaka 2017 kwa ufadhili kutoka nje ilikuwa ikitumia umeme wa jua (solar), mitambo yake iliharibika na kushindwa kufanya kazi.

Gilla alisema mwaka 2021 waliwasilisha maombi ya kijiji ili kupatiwa umeme wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) lakini mpaka sasa zahanati hiyo haijapatiwa huduma hiyo licha ya kijiji hicho kufikiwa na umeme huo.

"Kitu cha kushangaza REA imefikisha umeme kwenye kijiji cha Kiganila na tunawashukuru sana. Lakini kwenye zahanati pale mpaka sasa bado haujafika na kusababisha wajawazito kujifungua kwa tochi. Tatizo hili nimekuwa nikilisema sana katika baraza hili na leo narudia tena kwa kuwa kiongozi wa REA yupo hapa tunamuomba mtusaidie," alisema.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Lucas Lemomo, kabla ya kuruhusu mwakilishi wa REA kujibu hoja hiyo, alisema ni muhimu maeneo yanayotoa huduma za kijamii yakapewa kipaumbile.

Alisema halmashauri hiyo imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kuhakikisha inajenga zahanati pamoja na vituo vya afya ili wananchi wakiwamo wajawazito kupata huduma bora za afya.

Mwakilishi wa REA, Hilary Kuchapa, akijibu hoja ya diwani huyo, alisema suala hilo atalifikisha kwenye kikao cha juu ili liweze kupatiwa ufumbuzi wa haraka kwa kuwa yeye si mtoa uamuzi.

# MISA-TAN wajifungia kuimarisha usawa jinsia

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA TAN) kwa kushirikiana na Taasisi Inayoshughulika na Haki za Wanawake (VIKES) imefanya mkutano wa kuimarisha usawa wa kijinsia na uhuru wa vyombo vya habari.

Mkutano huo umefanyika kwa lengo la kuelekea Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake, yatakayofanyika leo.

Mkurugenzi wa MISA TAN, Elizabeth Riziki, akizungumza wakati akifungua mkutano huo, alisema lengo ni kuwaleta pamoja wahusika wa serikali, wataalamu wa vyombo vya habari na wawakilishi kutoka taasisi za kijamii.

Alisema lengo ni kuimarisha ushirikiano, kubadilishana mawazo, na kutafuta mikakati itakayochangia kukuza usawa wa kijinsia na uhuru wa vyombo vya habari.

Alisema mkutano huo unabebwa na kauli mbiu, "Kujenga Daraja: Mkutano wa Usawa wa Kijinsia na Uhuru wa Habari.".

"Malengo ya mkutano huu uliokutanisha Asasi za Kiraia, waandishi wa habari, serikali na wadau wa maendeleo ni kuweka jukwaa la kuwaleta pamoja wahusika wa serikali, wataalamu wa vyombo vya habari na wawakilishi wa taasisi za kijamii kujenga uhusiano, kubadilishana mawazo na kuchunguza ushirikiano unaowezekana," alisema.

Alitaja lengo lingine ni kujiandaa kwa Siku 16 za Uanaharakati Dhidi ya Dhuluma za Kijinsia kwa kuunganisha nguvu katika kampeni kubwa ya kimataifa ya siku hiyo na kuunda msukumo kwa juhudi endelevu zaidi baada ya tukio la siku moja.

Elizabeth alitaja malengo mengine ni kukuza usawa wa kijinsia kwa kushirikisha washiriki katika mazungumzo na mawasilisho yanayobainisha jukumu la vyombo vya habari katika kukuza usawa wa kijinsia.

Pia alisema kuupambana na dhuluma dhidi ya wanawake na kuhamasisha maendeleo ya ripoti na simulizi zinazozingatia masuala ya kijinsia.

Kadhalika alisema kukuza uhuru wa habari kwa kusisitiza umuhimu wa vyombo vya habari huru na visivyopendelea katika jamii ya kidemokrasia.

Alisema pia, kujadili changamoto zinazokabiliwa na wataalamu wa vyombo vya habari na kuchunguza njia za kulinda na kukuza uhuru wa habari.

# Maadhimisho ya Maalim Seif kutawaliwa na mijadala mizito

**Na Mwandishi Wetu**

MAADHIMISHO ya tatu ya maisha ya aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, yanayofanyika leo Visiwani Zanzibar, yanatarajiwa kubebwa na mijadala mizito ukiwamo ushindani wa kisasa ulioacha misingi na kujikita zaidi katika siasa 'chafu'.

Pia washiriki watajadili kuibuka kwa siasa walizoziita kulenga kucheza na akili za watu na kuwapa majibu mepesi kwa masuala mazito na athari zake kwa demokrasia.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Maalim Seif Foundation, Ismail Jussa Ladhu, lengo la mkutano huo ni kutafakari na kutathmini maudhui kwa kuangalia mwenendo wa siasa na uongozi kitaifa na kimataifa yakiwamo masuala ya kutetereka kwa maadili na misingi ya siasa na uongozi.

Jussa alisema kiongozi mashuhuri wa chama cha upinzani cha Build One cha Afrika Kusini (BOSA), Mmusi Maimane, anatarajia kuhudhuria maadhimisho yatakayofanyika kwa siku mbili.

Alisema mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, huku mtoaji wa salamu maalum atakuwa ni Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdullah.

Alisema maadhimisho hayo yatakutanisha viongozi mbalimbali wakiwamo wanasiasa, viongozi wa kidini, asasi za kiraia, wasomi, waandishi wa habari na wanadiplomasia huku maudhui ya mwaka huu ni, "Siasa, Uongozi na Utawala: Tumekosea Wapi, Tujisahihishe Vipi".

Alisema miongoni mwa mambo yatakayojadiliwa katika mkutano huo ni ushindani wa kisasa ulioacha misingi na kujikita zaidi kwenye siasa chafu.

Kadhalika alisema watajadili kuibuka kwa siasa zinazolenga kucheza na akili za watu na kuwapa majibu mepesi kwa masuala mazito na athari zake kwa demokrasia.

Hata hivyo, alisema wataalamu hao watajadili pia, siasa na uongozi katika zama za kidijitali na hasa mitandao ya kijamii namna ya kurejesha hamu na ushiriki wa rika la vijana katika siasa na uongozi.

"Pia kutajadiliwa namna ya kuainisha siasa na maendeleo ya nchi na masuala hayo yatachambuliwa na kujadiliwa kupitia uwasilishwaji wa mada na mijadala ya jopo yatakayowahusisha wanasiasa wazoefu, viongozi wa dini na asasi za kiraia, wasomi na waandishi wa habari, wanasiasa vijana,"alisema.

Alisema Jenerali Ulimwengu anatarajiwa kuongoza jopo la wanasiasa wabobezi ambao ni Profesa Kitila Mkumbo, Muhammed Aboud, Zitto Kabwe na Salum Mwalimu.

Wengine aliwataja ni Nicodemus Minde, Awadh Ali Said, Ezekiel Kamwaga, Absalom Kibanda, Maxence Melo, Hawra Shamte, Salma Said, Khalifa Said na Mohammed Ghassani.

Wengine ni Balozi Ali Karume, Hamza Kassongo, Prof. Mohammed Bakari, Sheikh Ponda Issa Ponda, Askofu Emmaus Mwamakula na Tike Mwambipile.

Wanasiasa vijana ambao watashiriki katika mjadala huo ni Rehema Sombi Omary, Mwanaisha Mndeme, Twaha Mwaipaya na mwanaharakati wa maendeleo Masoud Salim Mohamed.

Taasisi hiyo imekuwa ni jukwaa huru la majadiliano kwa kuwaweka pamoja wataalamu wa fani mbalimbali pamoja na kutoa elimu kwa vijana ikiwamo ukuzaji wa vipaji, ubunifu na uwezeshaji.

Hii ni mara ya tatu Taasisi ya Maalim Seif Fondation kuendesha mjadala na kuwakutanisha magwiji wa fani mbalimbali ambapo mwaka huu itakuwa na jumla ya washiriki walioalikwa 180.

Mkutano wa kwanza ulifunguliwa mwezi Novemba, 2021, na Rais Samia Suluhu Hassan ukiwa na maudhui ya mariadhiano na umoja wa kitaifa katika ujenzi wa Zanzibar na Tanzania mpya, mkutano wa pili ulifanyika mwezi Oktoba, 2022, ulikuwa na maudhui ya elimu na ukuzaji vipaji, ubunifu na uwezeshaji.

# Taasisi kuchangia wanafunzi mil. 600/-

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Dido Mwanafunzi Initiatives (DMI), imeandaa chakula maalum kwa lengo la kuchangisha Sh. milioni 600 kwa ajili ya kusaidia vifaa muhimu kwa wanafunzi wasiojiweza wa shule za msingi na sekondari katika mikoa minne.

Wanafunzi wanaolengwa ni katika shule za mikoa ya Mtwara, Geita, Njombe na Arusha ambapo watanunuliwa sare za shule, mabegi, soksi, viatu, taulo za kike na vifaa vingine muhimu.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Bodi ya DMI, Rehema Moses, alisema shughuli ya uchangishaji itafanyika leo jioni mkoani humo.

Alisema taasisi yake inatekeleza malengo hayo kama njia ya kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan katika kutoa elimu bila malipo na kuboresha mfumo wa elimu nchini.

"Licha ya mabadiliko haya chanya, wanafunzi wengi bado wanakutana na changamoto ya kukosa vifaa vya msingi," alisema Rehema.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Spectra Plast India Pvt Ltd, Ramkumar Servaraj (kulia), akizungumza na baadhi ya wateja waliohudhuria katika banda la India, kwenye maonyesho ya AgriTech Afrika Mashariki yaliyoandaliwa na Chemba ya Biashara na Viwanda ya India (ASSOCHAM), kwa kushirikiana na Serikali ya India, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waziri atishwa wimbi watumishi kutaka kuhama

**Na Lusungu Helela,** KILOLO

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, amesikitishwa na wimbi kubwa la watumishi, hususan walimu, wanaotuma maombi ya kutaka kuhama katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, Mkoani Iringa.

Kikwete alionyesha kutishwa na hali hiyo jana wakati akizungumza na watumishi wa halmashuuri hiyo ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kikazi mkoani humo ya kuzungumza na kusikiliza kero za watumishi na kuzitafutia ufumbuzi.

Alisema watumishi wengi wanaotaka kuhama wamekuwa wakitaja sababu zinazofanana, jambo ambalo lina walakini huku akisema kuna matatizo ya kiuongozi katika halmashauri hiyo.

Naibu Waziri alitaja moja ya sababu zinazofanya watumishi hao kutaka kuhama ni pamoja na kupuuzwa na kutokusikilizwa pindi wanapokuwa na changamoto.

"Kuna watumishi hapa hawajapandishwa vyeo kwa miaka tisa. Wengine hapa licha ya kujiendeleza kielimu, mishahara yao haijabadilika. Ninyi maofisa utumishi wenye jukumu la kufuatilia (Ofisi ya Rais) UTUMISHI na kuwapa majibu mpo tu. Hili si sawa hata kidogo," alisisitiza.

Kikwete alisema katika kalmashauri hiyo maofisa utumishi na maofisa tawala wamekuwa miungu watu badala ya kuwa suluhisho la matatizo yanayowakabili watumishi wanaowasimamia.

Alisema licha ya watumishi wengi wanaotaka kuhama kutaja sababu inayofanana kuwa ni uwepo wa baridi kali, hivyo kusumbuliwa na pumu jambo ambalo si kweli na ukweli ni kwamba hakuna uhusiano mzuri kati ya watumishi na uongozi wa halmashauri hiyo.

Kutokana na hali hiyo, Kikwete alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Estomin Kyando, kufanyia kazi changamoto zinazowakabili watumishi ikiwamo kufanya vikao vya mara kwa mara na watumishi kwa ajili ya kuwasikiliza na kuzingatia stahili zao zikiwamo posho za likizo.

Katika hatua nyingine, Kikwete aliwataka maofisa utumishi na maofisa tawala kuwa kimbilio la watumishi badala ya kuwa vikwazo katika kufanyia kazi matatizo yanayowakabili.

"Kazi yenu maofisa utumishi na maofisa tawala ni kusikiliza, kupendekeza watumishi wenu katika kupandishwa vyeo lakini mlio wengi mmekuwa watu wenye roho mbaya na mnaopenda kuwakomoa wenzenu. Acheni hizo," alisisitiza.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga hakuna timu nyepesi hatua ya makundi

**KWA** mara nyingine tena wawakilishi wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba na Yanga zote za Dar es Salaam, wikendi hii watashuka dimbani kusaka pointi muhimu za kuwania taji hilo kubwa kwenye ngazi ya klabu.

Yanga yenyewe jana usiku ilishuka ugenini Algeria kuanza hatua kwa makundi kwa kuwavaa wenyeji CR Belouizdad wakati Simba leo itakuwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kuwakaribisha ASEC Mimosas kutoka Ivory Coast.

Vinara na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga inacheza hatua ya makundi ya michuano hiyo baada ya miaka 25 kupita, inahitaji kufanya vizuri katika mechi zake za awali ili kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kusonga mbele sawa na Simba ambayo kwa misimu minne iliyopita imekuwa ikiishia hatua ya robo fainali.

Vigogo hao wa soka nchini, wanahitaji kuanza vyema hatua hiyo ili kujiongezea morali kuelekea michezo inayofuata lakini pia ikihitaji kumaliza kazi mapema badala ya kusubiri hadi mechi ya mwisho ili kufahamu hatima yao ya kusonga au kutolewa katika mashindano hayo yanayofanyika kila mwaka chini ya usimamizi wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Tunapenda kuwakumbusha Simba na Yanga kutodharau baadhi ya timu ambazo wamepangwa kundi moja na kuona nyingine kwao ni dhaifu na wanaweza kuvuna pointi kirahisi.

Kiukweli katika hatua ya makundi hakuna mechi rahisi, kila mechi kwenu iwe sawa na fainali, kila timu iliyofika hatua hiyo ni nzuri na inaweza kupata matokeo mazuri ama nyumbani au ugenini, kujituma na kucheza kwa nidhamu ni moja ya siri itakayowavusha na kuwapeleka hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo inayofanyika kila mwaka hapa barani Afrika.

Hatua ya makundi ni daraja lingine muhimu kwa wachezaji kujiweka sokoni kwa mawakala na makocha wa timu mbalimbali za Ulaya, kwa maana hiyo tunawakumbusha wachezaji wetu kuonyesha viwango bora ili kujiongezea thamani lakini pia kujihakikishia namba katika timu yao.

Kufanya vizuri katika mashindano haya, pia kutawasaidia wachezaji kupata namba ya kudumu au kuitwa katika vikosi vya timu za taifa, tunawakumbusha wachezaji kutochezea nafasi hii ya kushiriki hatua ya makundi kwa sababu huongeza thamani lakini pia huwaongezea uzoefu na uwezo wa kukabiliana na wapinzani wa aina mbalimbali.

Tunaamini kila mchezaji ana ndoto ya kusajiliwa na klabu kubwa duniani, lakini kung'aa katika hatua ya makundi kutawasaidia kuonekana katika vikosi vya timu za taifa katika fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2023), zitakazofanyika mapema mwakani huko Ivory Coast.

Huu ni wakati mwingine muhimu kwa wachezaji, viongozi na makocha wa timu hizi mbili kujipanga vizuri na kujiimarisha ili kufikia malengo ya klabu ya kubeba ubingwa wa Afrika, ndoto ambayo imekuwa ikisubiriwa na mashabiki wa soka hapa nchini.

Hakuna kisichowezekana katika soka, kikubwa ni kila mmoja kwa nafasi yake kutekeleza vyema majukumu na hatimaye matokeo chanya yatapatikana.

Nipashe inapenda kuwakumbusha wachezaji wa Simba na Yanga kucheza kwa nidhamu, kuacha kufanya makosa ambayo yanaweza kuigharimu timu yako na kukumbuka michuano hiyo inachezeshwa na waamuzi wenye uwezo mkubwa na ambao hawahofii na hawajui ukubwa wa majina ya klabu zenu.

Ni wazi makocha wa timu zote mbili tayari wameshafahamu uimara na mapungufu ya vikosi vyao, sasa wanatakiwa kutumia vyema kipindi cha dirisha dogo kujiimarisha kwa kusajili wachezaji wapya watakaosaidia kupata ushindi na kuwapa furaha mashabiki wenu.

Kila la heri Simba na Yanga ambao mnaendelea kupeperusha bendera ya Tanzania katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo kwa sasa yameingia kwenye hatua ya makundi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tanzania na kibarua cha kulinda nafasi nne CAF

Na Adam Fungamwango

**WAWAKILISHI** waliobaki katika michuano ya kimataifa, Simba na Yanga wameanza kampeni zao za kuhakikisha zinasonga mbele katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kinachofurahisha ni kwa mara ya kwanza katika historia ya soka la Tanzania, tangu nchi ipate uhuru, timu hizo mbili zinacheza kwa pamoja hatua ya makundi ya michuano hiyo, haijawahi kutokea na wala kudhaniwa huko nyuma.

Jana usiku, Yanga ambayo ipo Kundi D, ilicheza mechi yake ya kwanza baada ya miaka 25 dhidi ya CR Belouizdad ya Algeria, mechi iliyopigwa kwenye Uwanja wa Juillet wa Tano jijini Algiers.Mara ya mwisho Yanga kucheza hatua hiyo ilikuwa ni Novemba 8, 1998 dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast na ikapoteza kwa mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Taifa (sasa Uhuru), Dar es Salaam.

Simba, ambayo ipo kwenye Kundi B, leo itajitupa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kucheza mechi yake ya kwanza dhidi ya Asec Mimosas ikiwa pia ni mechi ya kwanza kwa timu hiyo.

Kwa upande wa Simba kwa sasa si habari kubwa sana kucheza hatua hiyo, kwani hii ni mara ya nne tangu 2019, na mara zote imekuwa ikiishia hatua ya robo fainali.

Haipingiki kabla ya Simba kufanya hivyo, Tanzania ilikuwa ikipeleka timu moja tu Ligi ya Mabingwa Afrika na moja Kombe la Shirikisho, lakini baada ya kufika robo fainali mara mbili, ilikusanya pointi ambazo ziliifanya nchi kupata wawakilishi wanne, ikiwa na maana wawili Ligi ya Mabingwa Afrika na wengine wawili, Kombe la Shirikisho.

Ndipo kwa mara ya kwanza tuliona hata timu ngeni, KMC ikipata nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho na Mtibwa Sugar nayo ikapata nafasi hiyo.

Baadaye Namungo, Biashara United nazo zilinufaika na hilo, achilia mbali Azam, lakini bahati mbaya tu uwakilishi wao haUkuwa mzuri sana.

Msimu uliopita, Yanga ikiwa katika mashindano ya Kombe la Shirikisho, ilifika hatua ya fainali na kuzoa pointi kadhaa ambazo zimeongeza uwezekano wa Tanzania kuendelea kunufaika kuwa miongoni mwa nchi zinazotoa timu nne katika michuano ya CAF.

Bila kujali matokeo ya mechi za mwanzo za Simba na Yanga katika makundi yao, lakini tunazitaka kupambana ambapo pamoja na kuzipa ushindi timu zao ili kuwafurahisha wanachama na mashabiki, pamoja na viwango vya klabu, lakini pia zinatakiwa kufanya hivyo kwa maslahi mapana na nchi. Kufanya vyema kwa timu hizo hakuzipi sifa timu hizo tu bali nchi kwa ujumla na ukitaka kuona hilo, angalia hivi sasa Tanzania imezidi nchi za soka kama Zambia, Kenya , Uganda na hata Rwanda ambazo zimebaki na mwakilishi mmoja Ligi ya Mabingwa na mwingine Kombe la Shirikisho.

Kwa kikosi ambacho Yanga anacho msimu huu, bila kujali matokeo ya mechi ya jana, lakini kina uwezo wa kutinga hatua ya robo fainali, huku Simba yenyewe ambayo inacheza leo kuingia hatua hiyo wala si stori tena, labda nusu fainali.

Binafsi nazitakia kila la heri timu hizo angalau zote zipite hatua hii ya makundi ili kutengeneza wigo mpana wa pointi. Inawezekana kabisa kama timu hizo zikipita hatua hiyo zinaweza kuvuna pointi ambazo zinaweza kusababisha timu za Tanzania kucheza hata misimu miwili bila ya kuwa na wasiwasi wa kupitwa na nchi zingine hata kama zikifanya vibaya.

Hilo ndilo linalopiganiwa na kuombea na Watanzania wote kwani ya mbele huwezi kujua. Kwa kipindi hiki ambacho timu hizi zina uhakika wa kufanya vema na vikosi bora ndiyo wakati wa kuweka wigo mpana wa pointi kwa ajili ya manufaa ya miaka ya mbele.

Timu za Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC), kwa sasa hazifanyi vizuri kwenye michuano hiyo, lakini kwa sababu kuna kipindi zililikamata soka la Afrika, kwa sasa inawalipa, hata kama zinatolewa mapema, lakini mwaka unaofuata zinakwenda nne.

Hili ndilo lipiganiwe kwa sasa na timu za Simba na Yanga na Watanzania wote wapo nyuma ya yao kuhakikisha hilo linatimia.




Rais wa Chama cha Waongozaji ndege Tanzania (TATCA), Merkiory Ndaboya (kushoto), akizungumza kuhusu jinsi chama hicho kilivyoweza kuwasimamia pamoja na kuwapatia elimu waongoza ndege nchini, wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa 43 wa TATCA uliofunguliwa na Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Uongozaji Ndege wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Hamis Kisesa, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Elimu fedha mtandao yatolewa kuongeza fursa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI tanzu ya Shirika la Mawasiliano Tanzania, T-PESA imetumia maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa kuelimisha wananchi kuhusu matumizi sahihi ya fedha mtandao na fursa zake ili waweze kujikwamua kiuchumi.

Ofisa Uhusiano wa kampuni hiyo, Adeline Berchimance, akizungumza katika maadhimisho hayo yanayofanyika katika Viwanja vya Shekhe Amri Abeid jijini Arusha, alisema wamefanya hivyo ili kuunga mkono jitihada za serikali za kusaidia jamii kujikwamua kiuchumi.

Maadhimisho haya yameandaliwa na Wizara ya Fedha na kuzishirikisha taasisi ndogo za fedha, benki, mifuko ya hifadhi za jamii pamoja na wajasiriamali.

"Katika kuunga mkono juhudi za serikali za kutatua changamoto ya ajira hasa kwa vijana, T-PESA inayofursa mbalimbali kwa vijana zinazoweza kuwasaidia kujitengenezea kipato na hivyo kujikwamua kiuchumi," alisema.

Alisema wameamua kutoa elimu kwa wananchi ili kuwajengea uelewa kuhusu matumizi sahihi ya fedha mtandao na fursa mbalimbali zinazopatikana katika kampuni hiyo zinazoweza kuwasaidia kujikwamua kiuchumi.

"T-PESA inazo fursa mbalimbali hasa kwa vijana ikiwa ni pamoja na uwakala ambapo wanaweza kufanya biashara na kujipatia kipato cha kusaidia familia zao," alisema Berchimance.

Pia alisema wameweza kujibu hoja, maswali na kero mbalimbali za wananchi kwa lengo la kuwaelimisha na kupata elimu sahihi kuhusu huduma na bidhaa wanazotoa.

Maadhimisho haya yanayofanyika kwa mara ya tatu sasa, kwa mwaka huu yamebebwa na kaulimbiu isemayo, "Elimu ya Fedha, Msingi wa Maendeleo ya Uchumi".

## KABWELA Na Fadhili Mohammed




# Polisi wafundwa utunzaji wa siri

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Kaspar Mmuya, amewataka watumishi wa Jeshi la Polisi kudumisha nidhamu na kutunza siri.

Vilevile, amewataka kufanya kazi kwa kutoa huduma bora kwa wananchi kwa kutenda haki ili jamii ifurahie hatua ambayo itadhibiti matukio mbalimbali ya kihalifu.

Akifungua Kikao cha 16 cha Baraza la Wafanyakazi wa Idara ya Jeshi la Polisi, Mmuya alisema hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan, ameliwezesha Jeshi la Polisi kwa kulipatia vitendea kazi ikiwamo magari kwa ajili ya kuongeza ufanisi mahala pa kazi.

Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini, IGP Camillus Wambura, alisema hali ya usalama nchini ni shwari na kwamba uhalifu umeendelea kudhibitiwa na wahalifu kufikishwa mahakamani hali ambayo imechangia kuongezeka kwa idadi ya watalii.

IGP Wambura alisema kupitia Baraza la Wafanyakazi wa Idara ya Jeshi la Polisi wamedhamiria kutatua changamoto, kujadili mafanikio na kupima ufanisi wa kufikia malengo ya serikali ya kuwa na Jeshi la Polisi la kisasa lenye mifumo imara ya kutoa huduma bora kwa wananchi.

# DAWASA yaipiga jeki shule madawati

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imekabidhi madawati 30 katika Shule ya Msingi Vikawe, Mkoa wa Pwani, kama sehemu ya kutambua na kuchangia ukuaji wa elimu katika jamii inayoihudumia.

Katika hafla ya makabidhiano iliyofanyika shuleni hapo wilayani Bagamoyo juzi, Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja DAWASA, Rithamary Lwabulinda, aliahidi ushirikiano zaidi kwa shule hiyo ili kuhakikisha wanafunzi wanasoma katika mazingira rafiki.

"DAWASA kupitia utaratibu wake wa kurudisha sehemu ya faida kwa jamii tumefanikiwa kutoa madawati 30 tukitambua mahitaji makubwa ya shule hii ili kuwezesha wanafunzi kusoma katika mazingira rafiki na waongeze ufaulu katika mitihani," alisema.

Lwabulinda alisema kwa sasa DAWASA ni sehemu ya jamii ya watu wa Vikawe, hivyo wataendelea kuwa bega kwa bega katika utoaji wa huduma na yatakapotokea mahitaji kadri itakavyofaa.

Mkuu wa Shule ya Msingi Vikawe, Jegama Selemani, aliishukuru DAWASA kwa msaada waliowapatia na kuomba isiwe mwisho wa uhusiano mzuri kati ya shule hiyo na mamlaka.

"Tulikuwa na mahitaji makubwa ya madawati, DAWASA wamechangia asilimia 40 ya mahitaji ya madawati, kwa hiyo wanafunzi 90 hawatasoma wakiwa chini tena," alisema.

Maulid Hamduni aliipongeza DAWASA kwa kazi kubwa inayofanya katika utoaji wa huduma ya majisafi lakini kwa kujali jamii inayoihudumia wakati inapokuwa na mahitaji.

"Msaada huu kwetu kama wazazi ni ahueni kubwa, wengi wetu tuna kipato cha chini na hata tunapojaribu kuchangishana muda mwingine hatufikii malengo. Madawati haya yatasaidia watoto wetu kusoma vizuri na kupata ufaulu wa hali ya juu," alisema Hamduni.

Vikawe yenye jumla ya wanafunzi 900 ni moja ya shule zinazonufaika na utaratibu wa DAWASA wa kurudisha kwa jamii sehemu ya faida yake.

# Mfumo unganishi kuondoa kero ardhi

**Na Munir Shemweta,**
ARUSHA

SERIKALI imesema mfumo unganishi wa kutunza taarifa za Ardhi unaoboreshwa na timu ya wataalamu jijini Arusha, utasaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa changamoto mbalimbali za sekta ya ardhi nchini.

Mfumo huo unaotarajiwa kuanza katika mikoa mitano ya Arusha, Dodoma, Mwanza, Mbeya na Tanga, utarahisisha na kuharakisha upatikanaji wa huduma za ardhi kwa kuwa wananchi watakuwa wakizipata kwa njia ya mtandao.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geofrey Pinda, alisema hayo juzi mkoani hapa alipokutana na kuzungumza na menejiment ya wizara na timu ya wataalamu inayooboresha mfumo huo.

Alisema sekta ya ardhi imekuwa na changamoto nyingi lakini hatua ya wizara kufanya maboresho ya kimfumo, itasaidia kuondoa kero na kelele za wananchi kwenye masuala ya ardhi.

"Kikubwa ambacho nimeanza kufarijika ni kwamba mmepiga hatua mpaka hapa mlipofika katika kuboresha mfumo. Hongereni sana baada ya muda tutakwenda kumaliza kelele za wananchi wa nchi hii," alisema Pinda.

Kupitia maboresho ya mfumo huo, alisema changamoto zote za sekta ya ardhi zikiwamo upatikanaji namba za malipo, malipo ya ada mbalimbali, upatikanaji hati, uthamini na migogoro ya ardhi, zitapatiwa ufumbuzi kwa njia ya kimtandao.

Kwa mujibu wa Pinda, itachukua muda mfupi kufikia malengo yaliyokusudia katika kuboresha mfumo huo kwa sababu kinachofanyika sasa ni kuwahamisha wananchi kutoka kwenye mfumo waliouzoea na kwenda katika teknolojia mpya.

Hata hivyo, amewatahadharisha wataalamu wanaoboresha mfumo huo pamoja na maofisa wa wizara kuwa makini kutokana na upinzani wanaoweza kuupata kutoka kwa baadhi ya watu aliowaeleza kuwa ni wanufaika wa mifumo ya sasa ambayo wizara itaachana nayo.

"Lazima mkawe 'standby' wakurugenzi na maofisa, wale waliokuwa wanakula kupitia mfumo wa kawaida mjue ndiyo tishio namba moja.

Wao ndiyo watakaoanza kusema mfumo wa ardhi bure kabisa lazima tutengeneze timu ya kukabiliana nao," alisema.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Lucy Kabyemera, alimweleza Pinda kuwa menejiment ya wizara imepitia kila hatua ya jinsi mfumo unavyofanya kazi lengo likiwa kufanya maboresho yatakayowezesha idara za wizara kutekeleza majukumu kwa ufanisi.

"Kupitia mawasilisho ya wataalamu tungetamani mfumo ukamilike mapema lakini kwa kuwa kazi hiyo inahitaji utaalamu, tunaamini itakamilika ndani ya muda mfupi," alisema Kabyemera.

Murugenzi wa Tekonolojia ya Habari na Mawasiliano wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na maendeleo ya Makazi, Flateny Hassan, alisema kutokana na wizara kuwa na changamoto kadhaa kwenye mifumo yake, imeonekana kuna uhitaji wa kuunganisha mifumo yote ili kuwa na mfumo mmoja utakaohusika na sekta nzima.

Alibainisha kuwa kazi kuboresha mfumo kwa sasa imefikia asilimia 75 na ni matarajio yake mapema Januari, mwakani, mfumo utaanza kutumika katika mkoa wa Arusha kabla ya kuendelea na mikoa mingine.

Hassan aliyataja maboresho yanayoendelea kufanyika kuwa ni pamoja na mfumo unaoruhusu watumishi wa sekta ya ardhi kutekeleza majukumu yao ndani ya ofisi zao, mfumo kuruhusu wananchi kuomba huduma kwa njia ya mtandao na huduma ya 'Mobile App' ambayo mwananchi anaweza kupata huduma kupitia simu ya kiganjani.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi St Mary's Tabata wakifurahi wakati Naibu Mkuu wa shule hiyo, Laizer Yassin (kulia), akiwajulisha kuhusu matokeo ya shule hiyo ya mtihani wa darasa la saba, shuleni hapo jijini Dar es Salaam jana, ambapo wanafunzi wake wote wamefanikiwa kufaulu kwa alama A. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Polisi waanza ukaguzi vyeti, leseni udereva

**Na Steven William**
MUHEZA

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani wilayani Muheza, mkoani Tanga, limeanza ukaguzi wa vyeti na leseni kwa madereva wote wa vyombo vya moto ikiwa ni utekelezaji wa maagizo kutoka makao makuu.

Uhakiki huo unafanyika katika stendi kuu ya mabasi wilayani Muheza Tanga na eneo la kijiji cha Kibanda barabara kuu ya Segera-Tanga mjini.

Mkuu wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Muheza, Leonard Bandola, ambaye anaendesha zoezi hilo alisema ukaguzi huo ni maagizo kutoka Makao Makuu ya Polisi.

Alisema uhakiki huo wa vyeti na leseni kwa madereva wa vyombo vya moto ni endelevu na atakayebainika kuchukuliwa hatua.

Bundala alisisitiza kuwa madereva wa vyombo vya moto wanatakiwa kuwa na vyeti vya udereva na leseni zao ili kuepusha usumbufu kwao.

Baadhi ya madereva wa vyombo vya moto, wamekiri kuwa kuna umuhimu wa madereva kuwa na vyeti vya kazi yao ikiwa ni pamoja na leseni.

Uhakiki wa leseni limeanza kwa kuzinduliwa na Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani Nchini, Ramadhani Ng'anzi, na kuendeshwa nchi nzima.

# Shule yafichua siri kufanya vizuri kwenye matokeo yake

**Na Joseph Mwendapole**

SHULE za St Mary's nchini zimeendelea kufanya vizuri kwenye mitihani ya darasa la saba kwa wanafunzi wake kupata wastani wa alama A kwenye matokeo yao.

Katika matokeo yaliyotangazwa jana na Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA), wanafunzi wote wa shule hizo wamefaulu kwa alama A na wachache wamefaulu kwa wastani wa alama B.

Mkuu wa Shule ya Msingi ya St. Mary's Tabata, Thomas Samson, alisema siri ya mafanikio ya shule hizo ni kuwa na walimu bora wanaotambua wajibu wao na kufanyakazi usiku na mchana kuhakikisha wanafunzi wanaelewa.

Alisema walimu wa shule hiyo wamefanyakazi kubwa ya kuwaandaa wanafunzi wake kwa kuwapa mitihani ya majaribio ya mara kwa mara hivyo wanafunzi wake kufaulu mitihani ya darsa la saba haijawashangaza.

Samson alisema walianza kuona dalili nzuri ya kufaulu kwa wanafunzi wa shule hizo baada ya kuwa wanafanya vizuri zaidi kwenye mitihani ya majaribio ya kimkoa na kiwilaya ambapo nako walikuwa wanapata wastani wa alama A.

"Sisi tunachojua ni kufundisha, mzazi ukitukabidhi mtoto wako ukae ukijua kwamba umemleta sehemu sahihi kwasababu hata kama angekuwa ni slow leaner tutamfundisha mpaka atakwenda na kasi ya wenzake wenye matokeo mazuri," alisema.

Naye Mkuu wa Shule ya Msingi St Mary's Mbezi, Isaac Tamaro, alisema amefurahi kuona wanafunzi wake wamefaulu kwa kiwango cha juu na kuahidi kuwa hawatabweteka na matokeo hayo na badala yake wataongeza juhudi.

"Siri ya ufaulu huu ni moja tu kufundisha na kuwawekea wanafunzi mazingira mazuri ya kujifunza kwa kuwapa vitabu vya kutosha na walimu wenye kujua wajibu wao kwamba ni kufundisha tu na kwa kweli matokeo ya juhudi zetu tumeyaona nawapongeza walimu," alisema.

Tamaro alisema wanafunzi wa shule za St Mary's wamekuwa wakipewa motisha mbalimbali wanapofanya vizuri ikiwemo kupelekwa kwenye mbuga za wanyama kama Mikumi, Serengeti, Ngorongoro na Ruaha kwaajili ya kutalii na kujionea wanyama mbalimbali.

"Tunaushukuru uongozi wa shule za St Mary's kwa kuendelea kujali walimu wake na kuweka mazingira mazuri ya wanafunzi kusomea binafsi naona hii imekuwa chachu ya mafanikio haya na tunawashukuru wazazi kwa kutuamini na sisi tunawaahidi kwamba tutaendelea kufanya vizuri zaidi," alisema.



## Wizara yashauriwa kuinua zao la ngano

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Daniel Mushi, ameiomba Wizara ya Kilimo kuhimiza wadau kutumia fursa za Jukwaa la Mifumo ya Chakula Barani Afrika kuinua uzalishaji wa zao la ngano nchini.

Dk. Mushi alitoa ombi hilo katika mkutano wa tisa wa Jukwaa la ANSAF uliofanyika jijini hapa.

Alisema ifike wakati wa kuipunguzia mzigo Serikali wa kutumia fedha nyingi kuagiza ngano nje kwa kuzalisha wenyewe nchini.

"Wizara ya Kilimo himizeni watu watumie fursa za Jukwaa la Mifumo ya Chakula barani Afrika ili kuinua kilimo cha ngano," alisema Dk. Mushi.

Alisema wanahitaji kuona kilimo kinakua kwa kasi nchini, hasa ikizingatiwa serikali imewekeza kwa kiasi kikubwa, hivyo jamii ijikite kwenye kilimo hicho.

Dk. Mushi, alisema Wizara ya Mifugo imefanikiwa kusafirisha tani 14 za nyama kwenda nje ya nchi na kuliingizia taifa fedha nyingi za kigeni.

Alisema inaonyesha jinsi gani Serikali inavyojitahidi kupanua wigo wa soko la nyama na mifugo ili wafugaji waweze kupiga hatua.

Alisema nchi nyingi zinazoizunguka Tanzania zinaitegemea katika mifugo, hivyo ni vizuri kujipambanua ili kusonga mbele na kuinua uchumi kwenye mifugo.

Mkurugenzi Mtendaji wa ANSAF, Honest Mseri, aliwataka washiriki hao kutumia walichojifunza kwa vitendo.

Alisema Serikali imeahidi kushirikiana na wadau wote, hivyo nao wajipange kutumia fursa inazotoa katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema jukwaa hilo likawe kielelezo kwa wakulima na wadau wa kilimo ili kuhakikisha wanatumia fursa za mkutano huo kupiga hatua.

# Tamisemi yawanoa maofisa tarafa, watendaji wa kata

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MAOFISA tarafa na watendaji wa kata mkoani hapa, wametakiwa kufanya kazi kwa kushirikiana ili kuondoa misuguano baina yao wakati wa kuwahudumia wananchi kwenye maeneo yao.

Wito huo umetolewa na Mhadhiri kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo mkoani Dodoma, Paul Faty, jana wakati akitoa mada kwenye mafunzo ya siku mbili ya kuwajengea uwezo maofisa hao yaliyoandaliwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Faty alisema mafunzo hayo yametolewa baada ya kubaini kuwa kumekuwa na mwingiliano katika utendaji kazi kwa maofisa hao na kusababisha kushindwa kufanya kazi ipasavyo ya kuwahudumia wananchi kutokana na sababu mbalimbali.

"Kufanya kazi kama timu na kushirikishana kutawafanya muwahudumie wananchi vizuri katika maeneo yenu kwa kusimamia utekelezaji wa sera, sheria kanuni na miongozo ya Serikali ," alisema.

Faty alisema moja ya majukumu ni kuwasikiliza wananchi na kutatua kero zao kwa sababu ndiyo waliopewa dhamana ya kuonana nao moja kwa moja na ni kiunganishi kati yao na serikali.

Mkuu wa Wilaya ya Singida, Paskas Muragili akifungua mafunzo hayo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema lengo ni kuwaongezea ujuzi na maarifa maofisa hao wa kutekeleza majukumu yao, kuondoa changamoto wanapo wahudumia wananchi na kuimarisha mahusiano baina yao na Serikali.

Muragili aliwakumbusha baadhi ya majukumu yao kuwa ni kumwakilisha na kumsaidia mkuu wa wilaya katika utekelezaji wa shughuli za Serikali na Taifa, kuhamasisha wananchi kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuwa kiungo cha wananchi.

Mkurugenzi Msaidizi Idara ya TAMISEMI, Hamisi Mkanga, alisema mafunzo hayo yalianzishwa kwa ajili ya kuwajengea uwezo maofisa hao kuanzia ngazi ya chini na kukiomba chuo hicho kiwatafutie mada watakazoendana nao.

Mkanga alisema mafunzo hayo yanafanyika kwa awamu ya baada ya katika mikoa ya Katavi, Rukwa, Njombe na Songwe.

Alisema katika awamu hiyo, mafunzo hayo yanafanyika katika mikoa ya Singida, Shinyanga, Tabora, Pwani, Dar es Salaam, Lindi na Mtwara.



Wakazi wa Makurunge, wilayani Bagamoyo mkoani Pwani, wakimsikiliza Wakili wao, Tenzi Anthony (kulia), wakati wakisubiri kuingia katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam jana, kusikiliza kesi ya Kikatiba waliyoifungua ya kupinga kuondoka katika makazi yao yanayodaiwa kuwa ni eneo la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Walalamikia TANROADS kutokuwalipa fidia Wananchi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ZAIDI ya wakazi 150 wa mitaa ya Chimala na Ntyuka jijini hapa, wamelalamikia Wakala wa Barabara nchini (TANROAD) Mkoa wa Dodoma kwa kushindwa kuwalipa fidia baada ya kupisha ujenzi wa mradi wa barabara.

Wakazi hao walidai juzi jijini hapa kuwa waliahidiwa kulipwa fidia Juni, mwaka huu, baada ya kupisha ujenzi wa barabara kuanzia Kata ya Ntyuka hai Kikombo, yenye urefu wa kilomita 76.

Mmoja wa wakazi hao, Michael Tengo, alisema waliahidiwa na TANROAD kulipwa fidia kabla ya ujenzi wa barabara hiyo kuanza.

"Tunaomba Rais wetu mpendwa atusaidie kwani shughuli zetu za uzalishaji mali zimesimama kwa muda mrefu na hatujui hatma yetu, na juzi walikuja kutuambia tunapaswa kubomoa nyumba zetu kwa hiari hili jambo linatuumiza sana," alisema Tengo.

Lightness Nkya alidai huenda kero hiyo inasababishwa na uongozi wa eneo hilo kwa kukosa ushirikiano na wananchi na kukataa kuzungumzia wanapoulizwa.

"Inawezekana kabisa labda suala hili lisingefikia hapa kama angetupa ushirikiano, hata tukimuuliza mambo yanavyoendelea huwa anakataa na kutueleza kuwa yeye siyo mhusika.

"Kwa hiyo naamini watu wengi tumekuwa tukiilalamikia Serikali kwa mambo mengi bila kujua watendaji wake wa chini ndiyo wanaoiangusha, tunaomba iangalie hili watu ambao imewaamini kuwa ni wawakikishi wake huku chini hawatusaidii sisi wanyonge, " alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ufuatiliaji wa malipo ya fidia, Athanas Matonya, alisema wana madai mengi ya fidia ya muda mrefu.

Alisema Serikali inapaswa iwaeleze bila ya kuwaficha kama haiwezi kuwalipa fidia baada ya kukaa kimya.

Diwani wa Ntyuka, Yona Andrew, alisema amefuatilia madai hayo kwa TANROADS bila mafanikio.

Endrew, alisema wananchi hao kwa sasa hawajui ni lini watapata stahiki zao na kubaki na sintofahamu huku ujenzi wa barabara ukiendelea.

"Wananchi hawa unaowaona hapo wana kilio cha takribani mwaka mmoja sasa tangu waahidiwe kulipwa fidia kutokana na shughuli mbalimbali ikiwemo kilimo baada ya maeneo yao kuchukuliwa na Serikali, hivi sasa wanadai kuambiwa waondoke na wengine kubomoa nyumba zao bila ya kujua hatima yao, "alisema.

Mhandisi wa TANROAD Dodoma, Calman Gaston, akizungumza na wananchi hao kwa niaba ya meneja wa mkoa aliwataka kuwa wavumilivu kwa kuwa malipo yao yanafanyiwa kazi na yakisha kamilika watapatiwa stahiki.





# Hospitali yafanya upasuaji kwa njia ya matundu Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

HOSPITALI ya Ampolo visiwani hapa, imeanza kutoa tiba ya teknolojia ya kisasa ya upasuaji kwa njia ya matundu.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake mjini hapa jana, daktari bingwa wa upasuaji mbobezi katika mfumo wa chakula wa hospitali hiyo, Alexander Mwelange, alisema wajawazito hawana kinga ya kupata magonjwa, hivyo upasuaji kwa njia ya matundu ni mzizi wa kutatua changamoto bila ya kuhatarisha uhai wa kiumbe kilichopo tumboni.

Dk. Mwelange alisema wajawazito hupata maumivu makali ya tumbo na baadhi yao huwa na vijiwe katika mfuko wa nyongo, kidole tumbo, vidonda vya tumbo, tiba yake ni dawa au kufanyiwa upasuaji ili kulea ujauzito huo usiharibike.

Alisema upasuaji wa matundu unaambatana na athari chache kwa mama na mtoto kuliko upasuaji wa kizamani ambao umekuwa ukiongeza athari za ujauzito kuharibika.

"Kidonda kinachotengenezwa na upasuaji wa kawaida ni kikubwa na mtu atakaa muda mrefu hospitali na kuongeza ujauzito kutoka, mgonjwa hupoteza damu nyingi, lakini upasuaji wa matundu, kidonda huwa kidogo chenye senti mita 1.2, unasaidia katika kuilea mimba hadi kufika muda wa kujifungua," alisema.

Daktari huyo alisema tiba ya njia za matundu ni salama na tangu waanze kutoa hospitalini hapo kwa muda wa miaka mitatu, kwa wiki wanahudumia wajawazito watatu.

Kwa mujibu wa Dk. Mwelange, upasuaji wa njia ya matundu hauna maumivu makali na wajawazito waliofanyiwa wapo salama na kupona matatizo yaliyokuwa yakiwakabili awali.

Alisema tiba ya upasuaji kwa njia ya matundu hufanyika pia kwa wanawake wasio na ujauzito na wanaume wenye changamoto za kiafya zikiwamo fumbatio, kidole tumbo na upasuaji wa mifupa. Dk. Mwelange aliwataka wajawazito na wananchi kupata ushauri wa matibabu hospitali na wasisubiri hadi ugonjwa unapokuwa sugu licha ya kuwa na dalili za awali. Alisema wanaume wanaongoza kwa kuchelewa kufika hospitali ikilinganishwa na wanawake kwa sababu wana shauku ya kutaka kujua kinachoendelea na kukosa kupata tiba kwa wakati mwafaka.

Daktari huyo, alisema kwa zaidi ya mwaka mmoja, hospitali hiyo inatoa tiba kwa watu wenye uzito wa kupitiliza kwa kutumia njia ya puto. Alisema zaidi ya watu 20 wamepatiwa huduma hiyo, wengi wao wakiwa wanawake.

Pia alisema hospitali yao ni ya kwanza kwa Zanzibar kutoa tiba kwa njia ya puto kwa watu wenye uzito wa kupitiliza.

"Hatusemi puto ndio mzizi wa fitina kwa wenye uzito wa kupindukia lahasha, lakini wanaokuja kutaka huduma hii tunawauliza upo tayari kwa huduma hii na umejaribu kufanya mazoezi na lishe bora umeshindwa ukisema ndio tunakupatia huduma ya puto," alisema.

Alisema tiba hiyo haina athari ya muda mrefu kwani ni sawa na athari za ujauzito za wiki ya kwanza kwa kutapika na kupatwa kichefuchefu na badala ya hapo hali inakuwa ya kawaida.

Meneja Masoko wa Hospitali hiyo, Edson Olotu, alisema wanatarajia kuwa na kambi maalumu ya uchunguzi na upasuaji wa magonjwa ya mifupa itakayoendeshwa na madaktari bingwa kutoa Dubai, Cuba na Tanzania kuanzia Desemba 1 hadi 17 mwaka huu.

# Watakiwa kupuuza taarifa za mitandao

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANANCHI wametakiwa kupuuzia taarifa za upotoshaji wa mjanga ya kiafya zinazosambazwa kwenye mitandao ya kijamii ili kujihakikishia usalama wa afya zao.

Hayo yalisemwa jana visiwani hapa na Mkurugenzi Kinga na Elimu ya Afya Zanzibar, Dk. Salim Slim wakati akifungua mafunzo ya kukabiliana na habari za upotoshaji wa majanga ya afya.

Dk. Slim alisema kuna upotoshaji wa taarifa za majanga ikiwemo magonjwa ya mlipuko katika mitandao ya kijamii na kuzua taharuki kwa wananchi.

Alisema mitandao ya kijamii imekuwa ikitumika kuzusha upotoshaji wa taarifa na kutoa nafasi ya kuenea kwa haraka kutokana na watu wengi kutumia kupata taarifa.

Aliwataka wananchi kuchukua tahadhari katika kipindi hiki cha mvua zinazoendelea kunyesha kwa kufuata taratibu zote za kiafya ili kuepuka magonjwa hayo.

Meneja wa Kitengo cha Elimu ya Afya Zanzibar, Bakari Hamad Magarawa aliwataka washiriki 110 wakiwamo wahuhudumu wa afya wa kujitolea kuyafanyia kazi mafunzo hayo yaliyoandaliwa na Shirika la Afya Duniani (WHO).




Meneja wa Kituo cha Kadi cha Benki ya NMB, Sophia Mwamwitwa (kulia), akizungumza na mmoja kati ya washindi 100 wa droo ya tatu ya Kampeni ya NMB MastaBata Halipoi, katika Tawi la Tegeta, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Ofisa kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), Pendo Mfuru na Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Tegeta, Peter Msaki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwinyi akaribisha wafanyabiashara kutoka China kuwekeza Pemba

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amewakaribisha wafanyabiashara wakubwa na wenye viwanda kutoka nchini China kuja kuwekeza visiwani humo.

Akizungumza juzi na Makamu Mwenyekiti wa Shirikisho la Wenye Viwanda na Wafanyabiashara wa China, Xu Lejiang na ujumbe wa wafanyabiashara 15 Ikulu, Zanzibar, Rais Dk. Mwinyi aliwaambia wafanyabiashara hao kuwa utalii ni fursa muhimu ya uwekezaji visiwani humo.

Alisema utalii hasa wa hoteli na maeneo ya kupumzikia una fursa nyingi za uwekezaji, na Zanzibar ina maeneo mazuri yenye fukwe nyeupe zinazowavutia watalii wengi.

Kuhusu sekta ya uchumi wa buluu, Rais Dk. Mwinyi aliwakaribisha wafanyabiashara hao kwenda kuangalia fursa zilizopo katika eneo hilo na Zanzibar, akisema mbali na sekta ya utalii inayoingiza asilimia 30 ya pato la taifa, uvuvi na ufugaji wa vifaranga vya samaki ni sekta muhimu pia kwa uchumi wa nchi.

Vilevile alisema maumbile ya visiwa vya Pemba na Unguja yana fursa adimu ya bandari, hivyo aliikaribisha China kuitumia fursa hiyo kwa uwekezaji, kutuma na kupokea mizigo baina ya nchi hizo.

Akizungumzia sekta ya mafuta na gesi, Dk. Mwinyi, alilitaka shirikisho hilo kuangalia eneo hilo kwa uwekezaji.

Lejiang alisema shirikisho hilo ni kubwa zaidi kwa China na limeyaweka pamoja zaidi ya makampuni makubwa na viwanda 700.

Alimwahidi Rais Mwinyi kuwashawishi wafanyabiashara wengi zaidi kuja kuwekeza visiwani humo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



**ASAP SASA MSHTAKIWA KAMILI** Ukurasa 14

JUMAMOSI NOVEMBA 25, 2023



# MIMI SIJAMUUA...

DUANE "Keefe D" Davis, amekana kuhusika na mauaji ya rapa maarufu nchini Marekani, Tupac Shakur, miaka 25 iliyopita.

Mtuhumiwa huyo ambaye ni mwanachama wa zamani wa genge hatari la Compton south Crips, kwa muda mrefu alikuwa akihusishwa na mauaji ya msanii huyo yaliyofanyika Las Vegas.

Septemba mwaka huu, Duane "Keefe D" Davis (60), alishtakiwa kwa mauaji hayo, ingawa ilidaiwa sio yeye aliyeshikilia silaha.

Awali alikiri kufanya mauaji hayo akidai kuwa alikuwa kamanda wa eneo hilo aliyetaka kulipiza kisasi kwa shambulio dhidi ya mpwa wake.

Akiwa katika mahakama ya Las Vegas, Davis alikana shtaka la mauaji kwa kutumia silaha kali kwa nia ya kukuza, kuendeleza au kusaidia genge lake la uhalifu.

Kulingana na sheria ya Nevada, tukio la kusaidia mauaji linaweza kusababisha mashtaka ya mauaji. Waendesha mashtaka wamesema kuwa hawashauri hukumu ya kifo ikiwa Davis atapatikana na hatia.

Tupac Shakur, msanii maarufu wa hip-hop, aliuawa Septemba 7, 1996, akiwa na umri wa miaka 25.

BASI SAWA

## ‘Too Sexy’ yampa kiburi Hennesseyy



BOSI wa lebo ya Spacious Music, Hennesseyy Hennesseyy, amezidi kupaa baada ya ngoma yake ‘Too Sexy’ kukamata namba za juu kwenye chati mbalimbali za muziki.

Hennesseyy ni miongoni mwa mastaa wa muziki wenye ushawishi kwa wasichana,amejizolea umaarufu kwa ngoma zake zinazochezeka na kufanya vizuri kwenye viwanja mbalimbali vya burudani.

Akizungumzia mafanikio hayo, amesema wimbo huo una siku 13 tangu utambulishwe, lakini unaongoza kwa kushika namba za juu kwenye mitandao ya kuuza na kusikiliza muziki ukiwamo YouTube.

“Tunaendelea kuachia projekti mfululizo ili kukuza muziki wetu na brandi ya Spacious Music tumewekeza pesa nyingi ili mashabiki wapate kitu bora,” amesema Hennesseyy.

## Rachel Angel alambisha ‘Jirani’ Mwanza



MWIGIZAJI anayekuja kwa kasi, Rachel Angel, amewashukuru mashabiki kwa kujitokeza kwa wingi katika uzinduzi wa filamu yake inayoitwa jirani uliofanyika jana ukumbi wa Boma, jijini Mwanza.

Akizungumza na BT jana, Rachel amesema yupo chini ya umoja wa Sangara Films, kundi ambalo lina kiu ya kuipaisha tasnia nje ya Mwanza na mipaka ya Tanzania.

“Filamu hii nimeshirikiana na mwenzangu ambaye yeye ni prodyuza mkuu ambaye tayari amefanya makubwa kwenye tasnia. Naamini filamu hii ya jirani itanitambulisha zaidi mimi pamoja na umoja wa wasanii tulioounda unaoitwa Sangara,” amesema Rachel.



## Harmonize sasa kazi tu

BAADA ya kupata mapokezi ya nguvu aliporejea nchini akitokea nchini Marekani ambako alitwaa tuzo tatu, mwanamuziki maarufu Harmonize, ameapa iwe jua au mvua atajikita katika kuutangaza muziki huo nje ya mipaka kwa nguvu zake zote.

Amesema huko nyuma alichanganyikiwa zaidi katika mapenzi, lakini sasa amegundua muziki unamuhitaji yeye kuuweka sawa na kuuweka katika kiwango cha juu kimataifa.

Ameongeza kwamba kinachosababisha watu kumpenda ni kutokana na juhudi yake kupambania Bongo Fleva na kuuweka kuwa miongoni mwa muziki pendwa duniani.





## Rayvanny ugomvi sio dili

MWANAMUZIKI Rayvanny amesema wasanii wanaohitaji mafanikio suala la ugomvi hawalipi kipaumbele kwa sababu litawarudisha nyuma.

Amesema yeye na Harmonize wameamua kuweka mambo sawa kutokana na kuweka maslahi ya mashabiki mbele na kwamba ukaribu wao uliokuwepo kwa sasa utaendelea kudumu.

“Mimi na Harmonize tumeshazeeka, wenzetu akina Rema wanajaza Arena ughaibuni sisi tunagombana hakuna maana, lazima tujifunze na kuweka maslahi ya mashabiki mbele kuliko yetu binafsi,” amesema.

## Tano mpya kali zinazotrendi Bongo

**Na Adam Fungamwango**

MWEZI Novemba unakaribia kwisha, lakini unaenda ukiwa na mambo mengi mema, kwani wasanii kibao wametoa ngoma zao kali ambazo kwa sasa zinaendelea kutrendi kwenye mitandao ya kijamii, redio na televisheni.

Hapa tuziangalie kwa uchache ngoma kali za wasanii maarufu ambazo zimeonekana kufanya vema kwa sasa.

**Commando-G Nako ft Diamond Platnumz**

Ngoma hii imefyatuliwa Novemba 13 na kwa muda mfupi tu imetrendi kweli kweli. Ni ya G Nako ambaye amemshirikisha mmoja kati ya wamuziki wa kizazi kipya Afrika, Diamond.

Mnaambiwa mlioachwa poleni, mnaodai poleni, msiyo na ‘baby’ poleni.

**Shuu-Aslay**

Novemba 15, msanii Aslay naye alipandisha ngoma yake mpya ambayo imeshika chati kweli kweli na mashabikiki huwaambii kitu.

“Yuko wapi aliyesema niko wapo? Aliyesema nitatetese-ka! Aliyesema sitompata kama yeye! Yuko wapi aliyekurusha roho? Yuko wapi, aliyetaka ukate roho? Yuko wapi aliyesema hutoishi bila yeye?” Ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye ngoma hiyo.

**Muda-Abdul Kiba ft Ali Kiba**

Ndugu wawili wameungana tena na kutoa ngoma kali wanayoiita ‘Muda.’ Wameitoa Novemba 16 na kwa siku chache mashabiki wa bongo fleva huwaambii kitu. Kwanza mashabiki wa Kiba, pili kuna wale ambao hupenda ndugu hao wakiungana na kutoa ngoma yao. “Nikiona pesa zinanipandisha midadi.” ni kipande cha maneno toka kwenye singo hiyo ya Abdul Kiba na Ali Kiba.

**Ahsante-Marioo**

Novemba 18, Marioo alitoa ngoma yake kali aliyoipa jina la ‘Ahsante.’ Hizi ndizo ngoma ambazo unaweza kupiga hadi kwenye mahafali ya shule za msingi au sekondari na isiwe kesi.

Ni moja kati ya ngoma chache siyo tu zisizo na lugha ya ukakasi, bali si za mapenzi kabisa.


Marioo anamshukuru Muumba wake kwa kumpitisha njia zote njema hadi kufika hapo.

“Mimi ni nani, ni yupi nisiyeweza, nisiyejua hata kushukuru?” Anasema Marioo kwenye ngoma hii ambayo imetrendi sana.

**Sijalewa-Harmonize**

Harmonize yeye mapema kabisa, Novemba 3 alipandisha ngoma moja kali ambayo imetrendi sana kwenye redio, televisheni na mitandao ya kijamii inayosema, ‘Sijalewa.’

“Huyo ex wako aliyenifanya ninywe nilewe mbona simuoni?” Anauliza jamaa.





## Mke jina: Jina marehemu

**Na Adam Fungamwango**

‘MKE Jina’, ni filamu inayoangazia familia hasa za Kiafrika ambayo kwa mtoto wa kike aliyezaliwa, kulelewa na kuwa mwali, ni lazima apate mume aolewe.

Kitendo cha kutoolewa kwa msichana huwa ni kama mkosi, laana na aibu kubwa kwa wazazi na ukoo mzima.

Mtoto wa kike kuzeekea nyumbani ni jambo ambalo kila mzazi huwa hataki limtokee.

Filamu imechezwa na Fadhili Msisili, Anifa Hanya, Edson Kalokola, Salha Ramadhani, Ashura Mashaka, na wengineo.

Asha ni msichana mzuri aliyeumbwa akaumbika, anayeishi kwenye kijiji kimoja nchini akiwa ni binti wa mzee Msisiri.

Pamoja na uzuri wake lakini hakuwa ameolewa. Kitu hicho kilimkera sana baba yake ambaye pamoja na kuona labda binti yake hatulii, lakini baadaye akafikiria kuwa kuna mkono wa mtu.

Siyo kwamba Asha hakuwa na mpenzi. Jumo ndiyo aliyekuwa mpenzi wake, lakini hakuwa amepeleka barua ya posa nyumbani kwao.

Asha anapomwambia mwenzake, akaambiwa mpaka kwanza wafanye mapenzi ndipo apeleke barua kwao, kitu ambacho binti alikuwa anapinga.

Kuna mwanaume anatoka mjini kuja kumuoa shoga yake Fatuma, hilo ndilo linamtia kabisa wazimu mzee Msisiri kiasi cha kufikiria kuwa huenda mama Fatuma anazuia mabinti wa wenzake wasiolewe.

Anamwita shangazi wake kutoka kijiji kingine kwa ajili ya kumpeleka mganga ili waangalie ni kwa nini haolewi.

Wanapofika huko mganga anawaambia kuna mama mmoja ambaye binti yake ameolewa ndiye anayefanya hivyo na anampa dawa.

Hali inaanza kuwa mbaya Asha alipokunywa dawa hiyo. Baada ya kuwa hoi taaban, binti anamwambia shangazi yake kuwa alichoka kuitwa mke jina, hivyo akaamua kufanya mapenzi na Jumo ikiwa ni sharti la kuja kutoa posa.

Kilichotokea ni kwamba tayari alikuwa mjamzito, na dawa chungu iliyotoka kwa mganga imekwenda kutibua kila kitu. Wakati Jumo ameshatimiziwa sharti lake na kupeleka barua ya posa nyumbani kwa mzee Msisiri kumuoa binti yake, hakumkuta. Alikuwa ameshafariki.



# Davido awapa presha mashabiki

MASHABIKI wa mwanamuziki kutoka Nigeria, Davido Adeleke, maarufu kama Davido, wameonekana kuzidiwa na hamu ya kuwaona sura ya watoto mapacha wa msanii huyo maarufu.

Davido ametimiza miaka 31 Novemba 21 mwaka huu, katika kuonyesha upendo aliweka picha katika ukurasa wake wa twitter akiwa amewabeba watoto wake huku akiwaficha sura zao.

Pia alionekana akiwa katika furaha zaidi kwa kumbusu mkewe, Chioma Rowland ambaye ni mama wa mapacha hao.



## Anuku hapo sawa, lakini ndo ulewe?

NYOTA wa Nollywood, Hanks Anuku amesema kwamba katika maisha yake yote hatumii dawa za kulevya za aina yoyote.

Mkongwe huyo aliweka video kwenye ukurasa wa Instagram akisisitiza kwamba amekuwa akikabiliana na mfadhaiko katika miaka michache iliyopita kutokana na kukosa ajira.

Anuku amesema kwamba kutokana na kuwa na huzuni amekuwa akinywa pombe lakini hatumii dawa za kulevya.

## Foxx jiandae kwa lolote

WANASHERIA wa mwigizaji wa Marekani Jamie Foxx, wanaendelea kujipanga kumuokoa mteja wao katika mashtaka ya kumnyanyasa kingono mwanamke mmoja jijini New York City miaka minane iliyopita.

Kulingana na kesi hiyo, Foxx, ambaye jina lake halisi ni Eric Marlon Bishop, inadaiwa alimpapasa mwanamke huyo ambaye jina lake halikutajwa baada ya kuomba apigwe picha naye.

Kesi hiyo inadai kuwa shambulio hilo lilitokea mwendo wa saa 01:00 asubuhi ya Agosti 26, 2015 katika eneo la Catch NYC baada ya mwanamke huyo kukaa kwenye meza karibu na Foxx.





## Diddy afichua alivyovunja benki

KUMBE rapa mkongwe wa Marekani Diddy ilimbidi avunje benki na kulipa kitita kikubwa cha fedha ili kujinusuru na kesi ya ubakaji.

Diddy alimpatia mpenzi wake wa zamani ambaye pia ni mwanamuziki Cassie kiasi cha dola milioni 30 katika usuluhishi wa nje ya mahakama.

Kama ilivyoripotiwa na TMZ, kesi hiyo ilitupwa na mahakama Jumatatu iliyopita baada ya Diddy kukubali kumlipa fidia.

## ASAP sasa mshtakiwa kamili

RAPA maarufu wa Marekani Rakim Athelaston Mayers, anayejulikana kama ASAP Rocky, sasa ni dhahiri anakabiliwa na shitaka la kumfyatulia risasi rafiki yake ASAP Relli mwaka wa 2021.

ASAP anatarajia kupanda kizimbani Januari 2024 huko Los Angeles baada ya ushahidi uliokusanywa kuonekana unatosha kumweka hatiani.

Kulingana na Jarida la People, Jaji M.L. Villar amesema wakati wa kesi ya awali iliyosikilizwa Jumatatu kuwa aliyekuwa rafiki yake wa karibu alidai kwamba alipigwa na risasi wakati yalipotokea mabishano kati yao.





# TADB yatangaza neema kwa wakulima

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), imewataka wakulima kwenda kuchukua mikopo kwa riba nafuu kwa ajili ya kuendeleza kilimo.

Rai hiyo imetolewa na Meneja Mawasiliano na Masoko wa TADB, Amani Nkurlu, wakati akizungumzia maonyesho ya huduma za kifedha yanayoendelea jijini Arusha.

"Kupitia TADB, wakulima wanaweza kupata mikopo ya muda mfupi, kati na mrefu kwa riba nafuu zaidi katika soko hadi kufikia asilimia tisa na tunatoa huduma zetu kwa wakulima na wafanyabiashara katika sekta ya kilimo kwenye mnyororo mzima wa thamani ikiwemo sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi," alisema Nkurlu.

Alisema TADB imeshiriki kwenye maonyesho hayo kama sehemu ya kuwafikishia wakulima fursa za mikopo ya riba nafuu, mafunzo na ushauri wa kitaalamu.

Kauli mbiu ya maonyesho hayo kwa mwaka huu ni 'Elimu ya Fedha, Msingi wa Maendeleo ya Kiuchumi' Wiki ya Huduma za Kifedha.

Maonyesho hayo hufanyika kila mwaka kwa lengo la kuwapa wananchi elimu ya fedha na kufahamu fursa, bidhaa na huduma zilizopo ili kujiongezea kipato na kukuza uchumi wa nchi.

Nkurlu alisema benki hiyo inashiriki maonyesho hayo kwa mara nyingine mwaka huu na kuwataka wakulima na wadau wa kilimo kuchangamkia fursa wanazotoa.

"Huu ni mwendelezo wa TADB kushiriki maonyesho ya huduma za kifedha na kwetu sisi maonyesho haya ni muhimu sana kwa kuwa hutuwezesha kukutana moja kwa moja na wakulima na wadau wa kilimo kutoka kila kona ya nchi," alisema.

TABD ilianzishwa mwaka 2015 kama taasisi ya maendeleo ya fedha kwa lengo la kuchagiza mapinduzi ya kilimo nchini. Baadhi ya huduma za benki hiyo ni pamoja na kutoa mikopo ya zana za kilimo, matrekta na ya miradi katika kilimo.

Benki hiyo inatoa mikopo kupitia Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo (SCGS) kwa kundi la wakulima wadogo kwa kushirikiana na mabenki washirika ya biashara ili kuhakikisha wakulima wadogo wengi zaidi wananufaika na mikopo ya riba nafuu.

# Watano mbaroni kujifanya maofisa TRA

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Arusha linawashikilia wakazi wanne wa jijini Dar es Salaam na mwanamke mmoja kwa tuhuma za kujifanya maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa lengo la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kutoka kwa wananchi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Fredy Malaki (34), mkazi wa Karakata, Francis Mwita (42), wa Ukonga, Fidelis Joseph (27), wa Msumi Mbezi, Celine Fortunatus (43) wa Temeke na Fereji Hamadi (40) wa mkoa wa Tabora.

Kamanda Masejo alisema watuhumiwa hao wanashikiliwa na Polisi kwa mahojiano zaidi na upelelezi ukikamilika jalada litapelekwa ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa hatua zaidi za kisheria.

Masejo ametoa wito kwa wananchi kujiridhisha na watu wanaofika kwenye maeneo yao ya biashara na kujitambulisha kuwa ni maofisa wa TRA kwa kuwahoji kwa kina kwa ajili ya kupata utambulisho wao halisi.

"Niwaombe wananchi wa Mkoa wa Arusha kutoa taarifa za baadhi ya watu hao wanaofanya matukio ya uhalifu hususani ya utapeli katika mkoa huu ili hatua kali za kisheria ziendelee kuchukuliwa dhidi yao," alisema.

Ofisa wa Kodi Mwandamizi wa TRA, Hamenyimana Ayoub, alisena mamlaka hiyo imekuwa ikipokea malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusiana na kuwepo watu wanaojiita maofisa wa mamlaka hiyo na kujipatia fedha kwa njia ya udanyanganyifu.

Alisema baada ya kupokea taarifa hiyo aliripoti Polisi na kufanikiwa kuwakamata watuhumiwa hao katika maeneo ya Manyara Kibaoni Wilaya ya Karatu mkoani Manyara wakati wakijaribu kutoroka.

John ambaye ni muhanga alidai kuwa watuhumiwa hao walifika dukani kwake na kujitambulisha kuwa ni maofisa wa TRA na kuanza kuwahoji huku wakitaka kulipwa sh. Milioni 4.5.

"Watuhumiwa hao walifika dukani kwangu na kujifanya maofisa wa TRA, huku wakitaka nitoe shilingi milioni nne bila kunipa sababu za msingi na baada ya kuwatilia shaka niliwasiliana na ofisa wa TRA kwa ajili ya kijiridhisha kama ni watumishi wao na walipofika kwa ajili ya kuwatambua wakiwa na Polisi walibaini ni matapeli," alisema.



Mkuu wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Leonard Bandora (kulia), akipata maelezo kutoka kwa mfanyabiashara wa vifaa vya ujenzi, eneo la darajani kwa Mwaka mpya, Habiba Issa (kushoto), wakati akikagua Daraja la Mto Amtico, baada ya kujaa maji ya mvua na kuharibu bomba kubwa la maji juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# TCRA 'yanadi' mfumo wa mawasiliano

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inaendelea kuhamasisha upatikanaji wa leseni kidijitali kupitia mfumo wa Tanzanite Portal ili kumrahisishia mtoa huduma za mawasiliano kuhuisha leseni kwa urahisi.

Ofisa Mwandamizi Mkuu wa TCRA, Semu Mwakyanjala, alisema hayo jana katika Wiki ya Huduma za Fedha inayofanyika kitaifa mkoani Arusha.

Mwakyanjala alisema hadi sasa leseni zinazotoa huduma za mawasiliano nchini ni 2,518, watoa huduma 1,531 na vyeti vya wanaothibitisha ubora wa vifaa vya mawasiliano 2,157.

Alisema katika hali ya kuendeleza huduma za kidijitali nchini, TCRA inatoa rasilimali adimu za masafa, namba na kikoa bure kwa wabunifu kwa ajili ya majaribio ya tafiti zenye tija kwa Taifa na jamii.

Pia alisema TCRA imeanzisha klabu za kidijitali nchini kuanzia shule za awali, msingi sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu ili kukuza ustadi wa kijiditi na teknolojia miongoni mwa wanafunzi kwa ajili ya kukuza bunifu za kisayansi zitakazotatua matatizo katika jamii.

Alisema klabu hizo zitakuwa zinajumuisha mafunzo ya programu kuhusu teknolojia za kijiditi, ubunifu, uvumbuzi kwa njia ya kompyuta, kujifunza jinsi ya kutumia programu za zana za kijiditali na miradi ya kiteknolojia kuhusu masuala ya kijamii na kiuchumi. "Kwenye klabu hizi vijana wanafunzi wanaweza kunufaika kwa fursa za semina zinazotolewa na wadau wa sekta, pia vigezo vinaweza kubadilika kulingana na klabu, shule au chuo, na mara nyingi tunashauri wanafunzi wajiunge kwenye klabu hizi, kwa hiyari na inaweza kuwasiliana na mwalimu wa jukumu la klabu au kiongozi wa klabu," alisema.

Alisema lengo la kuanzishwa kwa klabu hizo ni kuinua viwango vya matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) nchini na kuhamasisha vijana kuanzisha shule za awali, msingi, sekondari na vyuo vya kati na vikuu katika masomo ya sayansi na TEHAMA.

"Klabu hizi zitasaidia kutatua matatizo yaliyopo katika jamii kama vile wale waliobuni utumaji na kupokea fedha kwa njia ya simu za kiganjani, ambazo leo zimetusaidia kutuondolea usumbufu wa kutuma na kupokea fedha siku za nyuma," alisema. Aliagiza shule za awali hadi vyuo vikuu kuhakikisha wanafunzi wanakuwa na klabu hizo na mwongozo watapatiwa na TCRA wenye lugha za Kiswahili na Kiingereza.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Sekeseke la kipindupindu mara ya kwanza Bongo

## -Karantini nchi nzima, kusafiri kwa kibali maalum
## -Ukikutwa unakula embe unakamatwa

**Na Adam Fungamwango**

HAUKUWA mwaka mzuri kwa Watanzania, kwani majanga mawili makubwa yalitokea kwa wakati mmoja. Ni mwaka 1978.

Kwanza kabisa ni vita ya Kagera ambayo ilizuka baada ya kiongozi wa Uganda wakati huo, Nduli Idi Amin Dada kuvamia eneo la mkoa wa Ziwa Magharibi na kutangaza kuwa ni lake na litatawaliwa kijeshi kama inavyotawaliwa Uganda.

Hali hiyo ilisababisha Tanzania kuingia vitani kwa kulazimishwa, ili mradi tu kukomboa kipande chake cha ardhi kilichotwaliwa na Uganda.

Tanzania ikapigana na kukomboa Kagera, lakini pia ikaingia ndani ya Uganda na kutoa kipigo kikali hadi Amin akakimbia nchi.

Janga la pili ni ugonjwa hatari wa kipindupindu. Ni ugonjwa ulioua watu wengi nadhani kuliko hata vita ya Kagera kutokana sababu mbalimbali, kwani ndiyo ulikuwa unaingia kwa mara ya kwanza nchini.

Wananchi wengi hawakujua nini cha kufanya ili kuudhibiti, hivyo ilihitajika nguvu ya ziada na elimu na mambo mengine ili kuzuia vifo vya watu wengi.

Wakati ule familia moja iliweza kunawa maji yaliyokuwa kwenye bakuli moja. Anaanza baba hadi yule wa mwisho.

Watu walikuwa wakila matunda wakati mwingine bila kuosha na ilikuwa poa tu. Lakini ulipoingia ugonjwa huo ikawa ni marufuku kula tunda lolote, hususan embe mbivu ambayo inapendwa sana na inzi ambao ni kisababishi kikuu cha ugonjwa huo.

Hapo ndipo askari mgambo walipochukua chati. Wakaanza kutembea vijijini na sokoni kuhakikisha kwanza maeneo yote yanakuwa masafi, lakini pia kutomuona mtu yeyote akila ovyo njiani chochote kile, achilia mbali matunda.

Kitendo cha kukutwa unakula embe, au tunda lolote hadharani inaweza ikasababisha kukamatwa.

Watanzania ndipo walipoanza kujua neno karantini. Watu walizuiwa kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine kwa ajili ya kudhibiti maambukizo zaidi. Kusema kweli Watanzania waliteseka sana na ugonjwa huo mgeni.

Abiria walishushwa kwenye basi. Rafiki yangu mmoja aliniambia alipanda meli ya kwenda Mtwara, lakini ikifika Lindi hakuna abiria yeyote anayeteremka zaidi ya wale wanaotakiwa kushuka, yaani waliofika mwisho wa safari. Hakukutakiwa mtu yeyote ambaye anaendelea na safari akaruhusiwa kuteremka na kwenda kuzagaazagaa mitaani na kurejea tena wakati wa kung'oa nanga.

Kama nilivyosema ilifika wakati hakuna mtu wa mkoa mmoja kwenda mwingine bila kibali maalum.

Jamaa mmoja alisema alitembea kilometa zaidi ya 50 kwenda kwenye ofisi za mkoa wa Ruvuma kwa ajili ya kupata kibali maalum ili asafiri kwenda Dar es Salaam.

Na kilikuwa kinatolewa mpaka utoe sababu za maana za kwenda huko, kama ni kumtembelea mjomba, au ndugu hupewi.

Udhibiti uliwekwa kote, viwanja wa ndege, mabasi, treni na bandarini. Utaratibu wa maisha ya Watanzania na yeyote aliyeteremka ni lazima awe na kibali maalum.

Wakati huo serikali ilikuwa ikifanya juhudi mbalimbali za kuudhibiti, ikiwezekana kuutokomeza kabisa.

Ugonjwa huo ulibadilisha kabisa utaratibu na utamaduni wa Watanzania hata wa kusalimiana kwa kupeana mikono, kama ilivyokuwa corona.

Kilichowaogopesha zaidi ni wale waliokuwa wakifariki kwa ugonjwa huo, kwani mazishi yake yalikuwa tofauti na ilivyozoeleka.

Walizikwa na serikali kupitia kwa halmashauri zake mbalimbali za majiji na mikoa, ambazo wakati huo zilijulikana sana kwa jina la 'site.'

Kusema kweli hakikuwa kipindi kizuri kabisa, na wengi wanakikumbuka kwa matukio mbalimbali.

Ingawa mpaka sasa kuna wakati huzuka ugonjwa huo, lakini serikali imeshachukua hatua thabiti ikiwemo kuwepo kwa dawa, pamoja na kutoa elimu kwa wananchi, tofauti na zamani ambapo hata dawa zilikuwa za shida.









Wananchi nao kwa sasa wana uelewa mkubwa juu ya kuweka mazingira safi, hivyo unapozuka tu unadhibitiwa ghafla. Na hata hivyo huzuka kwa maeneo na si nchi nzima kama mwaka 1978.

Kipindupindu ni ugonjwa hatari unaosababishwa na bakteria hasa katika utumbo mwembamba. Bakteria hizo ambazo huitwa 'vibriocholerae', huweza kusababisha kuhara sana na kutapika sana pamoja na homa kali.

Maambukizi hutokea hasa kupitia maji au vyakula vilivyochafuliwa na wadudu kama vile nzi. Wadudu hao huweza kuchafua vyakula endapo vyakula hivyo vitaachwa wazi bila kufunikwa na chombo chochote na kuvutia inzi hao kutua juu ya vyakula hivyo na kuacha bakteria zitakazosababisha ugonjwa wa kipindupindu kwa mtu atakayekula chakula kile.

Uligundulika kwa mara ya kwanza 1816, na kuua watu wengi sana duniani

Kipindupindu hutokea hasa katika nchi pasipo maji safi, hasa ambako maji ya kunywa na majimaji ya choo yanaweza kuchanganyikana. Bakteria ya 'vibrio', 'cholerae', hupatikana hasa katika kinyesi na maji ya choo na pia katika maji ya bahari, maziwa na mito kama maji machafu huingizwa katika magimba ya maji bila kusafishwa kwanza.

Vilevile samaki na vyakula vingine kutoka maji yenye bakteria vinachafuliwa na vinaweza kusababisha maambukizo na hasa vyakula vinavyooshwa kwa maji yaliyochafuliwa na bakteria wa kipindupindu.

Tunakaribisha meseji kutoka kwa wasomaji ambao walishuhudia visa, mikasa, misiba iliyotokana na ugonjwa huo ulipoingia kwa mara ya kwanza na kutetemesha nchi nzima mwaka 1998.

**Tuma meseji 0716 350534**

# Usitishwaji mapigano waanza, watu washuhudia utulivu Gaza

**GAZA,** PALESTINA

MAKUBALIANO ya kusitisha mapigano kati ya Israel na Hamas yameanza kutekelezwa jana baada ya wiki ya saba za mahangaiko ya mashambuzi mabomu kutoka angani, majini na ardhini kulikumba eneo la Ukanda wa Gaza.

Kutokana na makubaliano hayo, mchana wa jana kulitarajiwa kuachiwa kwa mateka 13 wanaoshikiliwa na Hamas.

Makubaliano hayo ya usitishwaji wa mapigano yamepangwa kudumu kwa siku nne hadi 10, kulingana na mpatanishi mkuu nchi ya Qatar.

Pamoja na kuachiliwa huru kwa mateka hao, pia mamia ya wafungwa wa Palestina wanaoshikiliwa kwenye magereza nchini Israel wakiwamo wanawake na watoto wanatarajiwa kukabidhiwa kwa mamlaka ya Palestina.

Wakati hali ya utulivu imerejea kuanzia jana, kulishuhudiwa malori yaliyobeba misaada yakianza kuingia ndani ya Ukanda wa Gaza kupitia kituo cha mpakani cha Rafah.

Serikali ya Misri ilisema malori 200 ya misaada yataingia Ukanda wa Gaza kila siku katika kipindi chote cha makubaliano hayo, pamoja na uingizwaji wa lita 13,000 za mafuta ya dizeli na malori manne ya gesi.

Hata hivyo, vikosi vya jeshi la Israel vitaendelea kubaki eneo la kaskazini mwa Ukanda wa Gaza katika kipindi chote cha usitishwaji mapigano.

Kabla ya kuanza kwa makubaliano hayo, jeshi la Israel, IDF lilitoa onyo kwamba vita hivyo bado havijamalizika na kwamba watu wasirejee katika makazi yao eneo la kaskazini mwa Gaza.

Pamoja na kutolewa kwa onyo hilo, baadhi ya Wapalestina walianza kurudi eneo la kaskazini kwa kutumia usafiri wa mikokoteni na punda.

Umoja wa Mataifa unakadiria kwamba zaidi ya watu milioni 1.7 kati ya milioni 2.2, ambao ni wakazi wa Ukanda wa Gaza walikimbia makazi yao tangu vita vilipoanza Oktoba 7.

Karibu watu milioni moja wanaishi kwenye vituo vya wakimbizi vinavyosimamiwa na Umoja wa Mataifa Ukanda wa Gaza.

Katika hatua nyingine, Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF) lilisema maandalizi ya kuwapokea mateka yamekamilika.

Katika chapisho lake kwenye mitandao ya kijamii, IDF ilisema maeneo kadhaa yametayarishwa kwa ajili ya kuwapokea , ikiwa ni pamoja na msaada wa matibabu.

Baada ya mapokezi ya kupatiwa matibabu ya awali, mateka hao watahamishiwa katika hospitali mbalimbali nchini Israeli ili kuunganishwa na familia zao.

IDF pia limechapisha picha zinazooonyesha eneo la kuchezea lililowekwa kwa ajili ya watoto, mifuko ya matibabu na vifaa vingine vya kibinadamu.

Pia ilikuwepo helikopta moja ya kijeshi ya kuwabeba mateka hao wanaoshikiliwa na Hamas tangu ilipofanya mashambulio dhidi ya Israel.

Hali ya utulivu pia ilishuhudiwa katika eneo la mpaka kati ya Israel na nchi ya Lebanon tangu kuanza kwa utekelezwaji wa makubaliano hayo.

Kulingana na shirika rasmi la Habari la Lebanon, tangu kulipozuka vita hivyo, eneo hilo la mpakani limekabiliwa na mapigano makali kati ya jeshi la Israel na wanamgambo wa Hezbollah pamoja na makundi ya Kipalestina.

Hezbollah bado haijasema chochote iwapo itaheshimu makubaliano hayo, yaliyofikiwa chini ya uratibu wa Qatar kwa usaidizi wa Misri na Marekani.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani, Annalena Baebock alisisitiza haki ya Israel kujilinda.

Akizungumza kwenye kongamano la mwaka la chama chake cha Kijani, alisema Israel ina haki na wajibu wa kujilinda chini ya sheria ya kimataifa ya haki ya kuwalinda raia wake na kuongeza kamwe nchi hiyo haitakuwa salama ikiwa haitaudhibiti ugaidi.

Baerbock kwa mara nyingine alisisitiza kwamba Israel ilikuwa inapambana dhidi ya Hamas, na si Wapalestina na kwamba hata kabla ya vita, maisha ndani ya Ukanda wa Gaza yaligubikwa na umasikini.

**DW**

## Somalia yakubaliwa kujiunga EAC

**ARUSHA,** TANZANIA

JUMUIYA ya Afrika Mashariki imekubali ombi la Somalia kujiunga na kuitaka nchi hiyo kujiandaa kutia saini mkataba wa kukubaliwa hivi karibuni.

Hayo yalisema muda mchache uliopita na mwenyekiti wa Jumuiya hiyo Rais wa Burundi, Everiste Ndayishimiye ambaye muda wake unamalizika.

Katika mkutano wa viongozi wa nchi wanachama unaofanyika nchini Tanzania kuanzia jana, kikao cha leo, rais wa Somalia Hassan Sheikh alipokelewa rasmi katika jumuiya na katibu mkuu Peter Mathuki, ambapo mkataba ukishatiwa saini Somalia inakuwa mwanachama wa nane baada ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kujiunga mwaka wa 2022.

Kikao cha faragha cha marais kilichofanyika mapema Ijumaa, kimekubaliana pia kuhusu mkutano wa michango ambayo kila mwanachama anatarajiwa kutoa ili kuboresha shughuli za jumuiya.

Katika kikao cha leo, Rais Salva Kiir anakabidhiwa uenyekiti wa EAC.

Marais waliohudhuria, ni Mwenyeji Samia Suluhu wa Tanzania, William Ruto wa Kenya, Yoweri Kaguta Museveni wa Uganda, Hassan Sheikh wa Somalia ambaye ni mgeni maalum, Salva Kiir wa Sudan Kusini, na Evereste Ndayishimie wa Burundi.

Rais wa Rwanda na DRC wamewakilisha na wajumbe maalum wa marais wa nchi hizo.



Raia wa Kipalestina wakirudi katika makazi yao kaskazini mwa Gaza baada ya mapigano kusitishwa kuanzia jana.
**PICHA: REUTERS**

## Katumbi adai Rais Tshesekedi kashindwa kumaliza vurugu

**GOMA,** DRC

MGOMBEA wa upinzani katika nafasi ya urais katika uchaguzi mkuu nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Moise Katumbi amemshutumu Rais Felix Tshisekedi kushindwa kumaliza vurugu mashariki mwa nchi hiyo.

Akihutubia mkutano wa kampeni yake katika jimbo la Goma juzi, Katumbi alidai uzembe wa serikali ya Tshisekedi kushughulikia hali ya usalama katika jimbo hilo umesababisha watu kuishi kwa hofu.

Akiwa ameandamana na washirika wake wapya, waziri mkuu wa zamani Augustin Matata Ponyo, Seth Kikuni na Frank Diongo, aliwaambia maelfu ya wafuasi wake kwamba wakimchagua kuongoza taifa hilo atarejesha usalama katika mikoa ya Ituri na Kivu Kaskazini.

Katika mkutano huo wafuasi wa chama chake cha Ensemble pour la Republique, walionyesha hasira zao kutokana na kitendo cha jeshi la polisi kuwazuia kuingia uwanja wa ndege kumpokea.

Uchaguzi wa Urais nchini humo utafanyika Desemba 20, mwakani.

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT**
**CHANGE OF NAMES**
**BY DEEDPOLL**

BY THIS DEED, I MFAUME NASSAN KILINDO of Dar es salaam do hereby declare that the names MFAUME HASSANI are mine and that they have been used interchangeably in lieu thereof I was born and named MFAUME NASSAN KILINDO, whereas I do hereby assume and adopt the name MFAUME NASSAN KILINDO.

AND IN PURSUANCE of such change of name as aforesaid I hereby declare that I shall at all material times hereinafter in all records, deeds and instruments in writing and in actions, proceedings and in all dealings and transactions and upon all occasions whatsoever use and sign the name MFAUME NASSAN KILINDO as my name.

AND I HEREBY AUTHORISE and request all persons to designate and address me by such name of MFAUME NASSAN KILINDO.

I, the said MFAUME NASSAN KILINDO make this declaration conscientiously believing the same to be true in accordance with the provisions of Oaths (Judicial Proceedings) and Statutory Declaration Act 1966.

In witness whereof, I have hereunto set my hand this 09th day of November, 2023.

SIGNED by the said MFAUME NASSAN KILINDO who is known to me personally/identified to me by ... the latter being known to me personally this 09th day of November 2023

DEPONENT

BEFORE ME:

COMMISSIONER FOR OATHS



---

**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**IN THE DISTRICT COURT (DISTRICT DELEGATE) OF MANYONI AT MANYONI**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.10/2023**
**In the matter of the Estate of the late MARCO JOHN MSANDAE**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR GRANT FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**FLORIDA JOACHIM NTANDU...........PETITIONER**
**GENERAL CITATION (Rule75)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are here by cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above-named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 1 Day of December, 2023 of the publication of this citation in the newspaper.

Dated at Manyoni this 21 day of November, 2023.

G.F KAPAMA
RESIDENT MAGISTRATE
MANYONI

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

CLEMENCE STEPHEN MOSHA
Anatangaza kupotelewa na kadi ya Trekta , yenye namba za usajili T 722 CER Yenye Chassis Namba T 2184710, Engine Namba E2187660 Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .
Polisi Taarifa:
PHQ/KIL/MOS/5346/2023

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF RUNGWE DISTRICT AT TUKUYU**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 25595 / 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ELIAS DAMSON MWABEZA**
**AND**
**RODA MWANAHONJE MWABEZA.................APPLICANT**
**GENERAL CITATION (Made under rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filled on or before the 29th of November, 2023.

Dated at Rungwe this 16th day of November, 2023.

DISTIRCT RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE
RUNGWE - TUKUYU

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

NDUGU SHABANI MUSSA JUMA anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili T 116 DKU aina ya SUBARU,Rangi Nyeusi.Yenye Engine No.EJ20C006418 na Chasis No.BL5011578.
Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi namba
PHQ/DOD/DOD/RB/9744/2023

---

Victoria FINANCE

## TANGAZO LA MINADA YA HADHARA

VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | NYARAKA YA UMILIKI NA SEHEMU | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | CHRISTOPHE R B. UHAGILE | NYUMBA | HATI YA MAUZIANO - KIHANGA RUJEWA | HOLINESS & RESPISHERS | 09/12/2023 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika vyombo husika vya Serikali.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.151 OF 2023**
**In the matter of the Estate of the late VENANCE JOSEPHAT KABULA of Kondoa within Dodoma Municipality**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY JANE VENANCE KABULA**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above-named deceased Person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above-named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before the 15 Day of 12, 2023

Dated at Dodoma this 06th day of November, 2023

..................................................................
**PETITIONER**
**Presented for filing this 24 day of November 2023**
..................................................................
**RESIDENT MAGISTRATE**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.126 OF 2023**
**In the matter of the Estate of the late WALUKO CHIMATA MNYAMBWA of Ipagala within Dodoma City**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ANDREA MALIMA CHIMATA**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above-named deceased Person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above-named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 6 Day of 12, 2023

Dated at Dodoma this 15 day of 11, 2023

..................................................................
**RESIDENT MAGISTRATE**

RESIDENT MAGISTRATE

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.142 OF 2023**
**In the matter of the Estate of the late AGNES EZEKIEL YOHANA**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY AMANI NOEL CHARLES**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above-named deceased Person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above-named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before the 13rd Day of 12, 2023

Dated at Dodoma this 17th day of October, 2023

..................................................................
**PETITIONER**
**Presented for filling this 22nd Day of November..........2023**
..................................................................
**MAGISTRATE**

---

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**
**Piga Simu 0677020701**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 745 700 710***

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**Website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HADITHI

# HADITHI

MWANTUMU, au mama Mwadawa, ni mwanamke ambaye muda wote yeye anachowaza ni umbea, ugomvi na kufitinisha watu. Anawagombanisha majirani wasielewane, ndoa za majirani zake nazo haziko salama hajaziacha, kwani amekuwa akizitikisa. Kwa bahati mbaya au nzuri anaishi kwenye nyumba ya urithi ya marehemu mama yake, yeye akiwa ndiye mama mwenye nyumba. Cheo hicho cha Umama wa Nyumba asiyojenga, ndiyo akawa amepata fimbo ya kuwapigia watu. Wapangaji wanaopanga kwenye nyumba hiyo wamekuwa wakiishi kwa amri, manyanyaso, kufokewa kama watoto wadogo. Ndani ya nyumba hiyo, wapangaji wamekuwa kama wakiishi bure au kwa mama wa kambo, huku silaha yake kubwa ikiwa ni kuwatishia kuwahamisha. Hebu fuatilia mwanzo na mwisho wa visa vya mama huyu.

# Mama mwenye nyumba-**3**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**




"Kwanza nilitaka kukufuata nikupe taarifa ya shughuli shoga, miezi miwili ijayo, dada yangu Mkuranga anaozesha, halafu nikupe umbeya."

"Umbeya wa nani tena?"

"Wako wewe mwenyewe. Wanavyokuongelea. Yaani shoga yangu ukiwa unaongea na watu, ukiwapa kisogo tu, wanakung'ong'a."

"Mimi hiyo?"

"Kwani kuna Bishada wawili? Si yupo mmoja tu ambaye ni wewe!"

"He, niambie koma!"

"Wanakuongelea vibaya dada yangu, yaani wewe hapo huna nguo."

"Shoga yangu mama Amina yasiwe ya uongo maana wewe una maneno sana, nakufahamu fika!"

"Wala! Shoga yangu Bishada mimi siwezi kuongea maneno ya uongo na wala nikisikia watu wanakuteta, siwezi kumezea, nimeona nije kukupa ubuyu."

"Sasa shoga yangu, saa hizi napeleka marejesho ya vikoba, njoo jioni saa 12 utanipasha kwa utuo, na nataka nijue vikaragosi gani hao waliokwambia maneno hayo. Hawana hata haya."

Ukweli ni kwamba hakukuwa na umbea wowote. Mwantumu alitumia mbinu hiyo ili kumpunguza munkari Bishada kwani alikuwa ameshawaka kwa ajili ya kucheleweshewa kurejeshewa kuazima taiti yake, gauni na blauzi alivyomuazima. Taratibu akarudi nyumbani kwake.

*******************

"Enhee kikaragosi gani aliyesogeza nguo zangu?" Lilikuwa ni swali la kwanza baada ya kufika nyumbani kwake.

Muda wote alikuwa amekaa kisharishari tu. Nguo alizoanika zilikuwa zimekauka, hivyo mpangaji wake mmoja aliona azisogeze kidogo ili na yeye aanike kwenye kamba. Hakuna aliyejibu.

"Nauliza tena, huyu mwanamke ambaye hajafundwa aliyetoa nguo zangu nilizoanika akaanika yeye ni nani?" Kwa mara nyingine hakukuwa na jibu.

"Narudia kwa mara ya tatu, huyu aliyeona nguo zake za maana, akasogeza za kwangu akaanika zake ni nani ajitokeze kabla sijafanya yangu!" Akaendelea kufoka.

"Ahaa hamjibu eee, sasa subiri niitupe chini hii mitambaa."Kabla hajafanya hivyo akatokea mpangaji mwingine na kuanza kuzuia zoezi lile.

Alikuwa ni Tabia, mmoja wa wapangaji wake. Yeye hakuwa na mume, alipanga peke yake. Kazi yake ilikuwa ni mhudumu kwenye baa moja, Magomeni Mapipa.

"Yaani we mtoto mdogo hata kunyonya hujaacha ndiyo unafanya hivi?. Nakwambia usinitafute la rohoni nikaonekana mbaya." Akafoka kwa ukali.

"Kilichokufanya utundike hii mitambara yako wakati kulikuwa na nguo zangu nini? Kwa nini umesogeza nguo zangu kwa sababu ya hii midekio yako?"

Tabia akaja kwa hasira, akaanua nguo zake ambazo zilikuwa bado mbichi ili amuchie mama mwenye nyumba kamba aendelee kuanika zake yeye ambazo zimeshakauka.

"Basi nikwambie ya kwako ndiyo matambara, ndiyo maana nikaanika za kwangu za maana." Tabia akajibu kwa jeuri huku akiondoka na nguo zake mbichi mkononi.

"We mwana wee, sitaki wapangaji jeuri kwenye nyumba yangu."

"Si nimekuachia kamba yote ili uanike vizuri!" Tabia akajibu kwa hasira akiwa mlangoni anaingia chumbani mwake.

Akijua kabisa kuwa nguo zake zimekauka, Mwantumu au mama Amina alizitandaza tena na kuzianika kwenye kamba ili kuendelea kuzuia wapangaji wake wasianike.

Kwa bahati mbaya wakati anaanika ya mwisho kabla ikakatika. Nguo zikaanguka chini. Bahati tu zilikuwa zimekauka. Akaona huu sasa ndiyo wakati wa kumtengenezea mtu kesi.

Akapiga hatua hadi kwenye mlango wa chumba cha mpangaji wake Tabia.

"We Tabia, yaani hasira zako mpaka unatukatia kamba, sisi tukaanike wapi?"

"Nini?" Akauliza Tabia.

"Toka huku nje uone ulivyofanya!" Mama mwenye nyumba akaongea kwa sauti ya juu.

Tabia akatoka nje, halafu akaonyeshwa kidole kuelekea kwenye kamba, "nini kile?"

"Toba, yaani wee mama umeamua kukata kamba ili unisingizie mie!? Akashangaa Tabia na kuuliza kwa wakati mmoja.

"Wewe ndiye uliyekata. Umeanua matakataka yako kamba ikakatika. Nakuita ukaingia ndani."

Wakati akiongea maneno hayo, Mwantumu alikuwa mbali kidogo na Tabia. Tabia damu ikamchemka. Alijua kabisa kuwa yeye siye aliyefanya hivyo. Alianua nguo zake vizuri tu hadi anaingia ndani, na kumuacha mama mwenye nyumba akirudishi za kwake.

Akataka kwenda kumvamia mama mwenye nyumba. Devota aliyekuwa amekaa kwenye mkeka alikijifumua nywele ni kama alijua mpangaji mwenzake atafanya vile. Ghafla akainuka na kwenda kumzuia. Tabia alikuwa ameshafika katikati ya pale alipokuwa amesimama awali na alipokuwa Mwantumu.

"Basi basi tabia acha, epusha balaa." Devota akamsihi. "Niache, niache niende nikamuonyeshe mbwa yule." Tabia alikuwa anafanya juhudi za kujipapatua kutoka kwenye mikono ya mpangaji mwenzake kwenda kumshikisha adabu mama mwenye nyumba.

"Mbwa mwenyewe, njoo njoo uone nitakavyokufinyanga kama unga wa ngano, hayawani mkubwa we." Akajibu Mwantumu kwa juhudi zote.

Muda huo huo, tayari kundi la kinamama, wapangaji wa nyumba hiyo, nyumba jirani pamoja na watoto kibao walitinga kuangalia nini kinaendelea baada ya kusikia kelele za majibizano.

Kama kawaida ya wakazi wa uswazi. wasisikie kitu. Wakajazana kibao, kushuhudia kinachondelea.

"Devota ungeniacha kwanza niende kumfundisha adabu huyu mwanamke. Mama mwenye nyumba gani. Wakati hujaja hapa tuliishi vizuri, kosa tu wewe kukanyaga, watu hatuelewani. Wapangaji kila siku roho juu juu kama tumeua mtoto wako!"

Devota tayari alishapata msaidizi mwingine wa kumzuia Tabia.

"Tabia acha msimkaribishe shetani." Mama mmoja wa makamo aliyekwenda kumsaidia Devota kumzuia Tabia.

Kuona hivyo mama mwenye nyumba aliingia ndani. "Bahati yako, mshukuru Devota, ningekung'oa meno leo, mwanga mkubwa wee." Tabia alimsindikiza na maneno.

"Mwanga mwenyewe. Haya nimetoka sasa nilikwenda kukuvalia pensi ndani, njoo tupigane na nakwambia mkataba wako ukiisha sikutaki uhame, nimekuchoka mbwa we."

"Siyo mkataba ukiisha kama unazo pesa nirudishie kodi yangu niondoke, hata mimi nimechoka. Nyumba gani hii kila siku ugomvi. Kama hakuna nyumba ya kupanga niende hata nikaombe kuishi gerezani kwa muda wakati natafuta chumba kuliko hapa. Na kilichonifanya mimi nihamie hapa sijui kitu gani?"

"Umasikini wako, ungejenga ya kwako!" Mwantumu akadakia.

"Wewe ya kwako? Si umerithi tu ya mama yako. We mwenyewe una ubavu huo? Hali yako ya mkunga ukijikuna unatoka unga, una ubavu huo?"

"Nyinyi mnamuona huyu ananitukana eee. Nakwambia leo natoa makochi yako mabovu nje."

"Thubutu, bila kunirudishia kodi yangu? Nipe kodi yangu kwanza uone kama nitang'ang'ania kijumba chako kibovu hiki."

"Mbona unakaa?"

"Mimi nilijua? Si nililetwa na madalali tu. Nasubiri tu kodi yangu ikiisha kama utanione."

Hali ilizidi kuwa mbaya, kiasi kwamba ilionekana kama wanawindana. Devota na mama wa jirani, walimvuta Tabia na kumuingiza chumbani kwake, wakafunga mlango kwa nje.

"Utawaonea wapangaji hao hao wanaokutetemekea siyo mimi!"

"Kelele, baamedi mkubwa we." Mama mwenye nyumba naye akajibu.

**Wakati akiongea maneno hayo, Mwantumu alikuwa mbali kidogo na Tabia. Tabia damu ikamchemka. Alijua kabisa kuwa yeye siye aliyefanya hivyo. Alianua nguo zake vizuri tu hadi anaingia ndani, na kumuacha mama mwenye nyumba akirudishi za kwake.**

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# SERIKALI YAONGEZA NGUVU SAFARI YA TWIGA STARS CAF

**Na Saada Akida**

SERIKALI kwa kushirikiana na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), imesema itaongeza nguvu katika kuhakikisha Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), inafanya vizuri katika mchezo wake wa mwisho wa kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (WAFCON 2024), imeelezwa.

**Fainali zijazo za WAFCON zitafanyika mwakani nchini Ivory Coast.**

Tayari kikosi cha Twiga Stars kimeingia kambini juzi ili kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa raundi ya tatu dhidi ya Togo utakaochezwa Novemba 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam, Dar es Salaam huku timu hizo zikitarajiwa kurudiana Desemba 5, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mtendaji wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Neema Msitha kwa niaba ya Katibu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, alisema Serikali kwa sasa imeelekeza akili na nguvu zake kuhakikisha Twiga Stars inashinda mechi zote mbili na kusonga mbele katika michuano hiyo.

Msitha alisema wanafahamu mechi hiyo itakuwa na ushindani kwa sababu wanakutana na timu yenye uzoefu, lakini anaamini umoja utasaidia kufikia malengo.

Alisema mechi dhidi ya Togo ni kubwa kwa sababu ni mchezo wa mwisho wa kutafuta tiketi ya kufuzu kushiriki fainali hizo na wanahitaji kuona wanashinda kwanza hapa nyumbani kabla ya kwenda kumaliza kazi ugenini.

"Huu ni mchezo muhimu sana kwetu kushinda kwa sababu tutakuwa nyumbani, tunahitaji kushinda na kumaliza kwanza kazi katika mechi hii ya nyumbani ili tutakapokwenda kurudiana basi safari yetu isiwe ngumu.

Tunatambua ubora wa hii timu yetu, tukumbuke mwaka 2010 tulienda kucheza fainali hizo Afrika Kusini, sasa tunataka kwenda kwa mara ya pili mwaka huu baada ya kaka zao (Taifa Stars) kufanikiwa kwenda AFCON," alisema Msitha.

Amewaomba Watanzania kujitokeza kwa wingi uwanjani kuisapoti Twiga Stars kwa sababu anaamini kufanya vizuri kwao ni kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania.

Naye Mkurugenzi wa Sheria, Habari na Masoko wa TFF, Boniface Wambura, alisema kwa kushirikiana na serikali watahakikisha timu hiyo inakuwa katika mazingira mazuri kuelekea mchezo huo.

"Hii ni safari yetu muhimu ya kwenda kucheza fainali ya pili ya WAFCON baada ya miaka 13 , mara ya kwanza tulienda kucheza Afrika kusini, sasa tunahitaji kushinda mechi yetu ya Novemba 30 hapa nyumbani.

Tunahitaji kushinda nyumbani na baadaye kwenda kumaliza kumaliza kazi ugenini ili kusaka tiketi hiyo muhimu ya kucheza fainali ya WAFCON," alisema Wambura.



Mshambuliaji wa Namungo FC, Reliant Lusajo (katikati), akijipanga kuwatoka wachezaji wa Ihefu katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Majaliwa, Lindi juzi usiku. Namungo walishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# Ladies First mambo kumekucha

**Na Saada Akida**

MASHINDANO ya riadha ya wanawake yajulikanayo kwa jina la 'Ladies First' yanatarajiwa kufanyika leo kwenye viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru, Dar es Salaam.

Katika kuhakikisha mashindano hayo yanayoshirikisha wanariadha wanawake kutoka mikoa yote nchini yanafanyika vyema, waamuzi wametakiwa kusimamia vizuri kwa kuzingatia sheria na kanuni ili kutimiza lengo la kupata vipaji vipya.

Wanariadha watakaoshiriki watachuana katika mbio za mita 100, 200, 1000, 1500, 2000, 5000 na 10,000 pamoja na kurusha mkuki na mshale.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Michezo wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Charles Maguzu, alisema waamuzi wanatakiwa kuacha kupendelea na kufuata sheria na kanuni za mchezo huo.

"Semina mliyopewa mnatakiwa kuzingatia kipindi mnasimamia mashindano haya kwa sababu tunagemea kupata wanariadha bora ambao watakuja kulitangaza taifa katika mashindano ya kimataifa, "alisema Maguzu.

Mwanariadha mkongwe nchini, Juma Ikangaa, ambaye ni balozi wa Shirika la Maendeleo ya Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA), alisema lengo la mashindano hayo ni kukuza na kuendeleza vipaji vya wasichana hapa nchini.

"Mashindano haya yatawapa nafasi ya wasichana kuonekana kwa sababu hakuna mashindano ambayo wanatoa fursa ya kuonekana na kufikia matarajio yao, Ladies First itawasaidia kuonekana na kuendelea kupata nafasi ya kuitwa kwenye timu za taifa," alisema Ikangaa.

# U-18 yaahidi neema michuano CECAFA

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Timu ya Soka ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 18, kimeahidi kurejea na ubingwa wa mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-18), yanayotarajiwa kufanyika kuanzia leo hadi Desemba 4, mwaka huu nchini Kenya.

Wenyeji Kenya watawakaribisha Sudan katika mechi ya ufunguzi ya Kundi A wakati mapema asubuhi Somalia itavaana na Rwanda, mechi zote zikichezwa katika Kituo cha Kisumu.

Tanzania Bara iliyoko katika Kituo cha Kakamega, imepangwa Kundi B ikiwa pamoja na Uganda, Sudan Kusini na ndugu zao Zanzibar.

Akizungumza kuelekea mashindano hayo, Kocha Mkuu wa timu ya Tanzania Bara, Habib Kondo, alisema wachezaji wake wamejiandaa vyema na wanaahidi watapambana katika kila mechi ili kupata matokeo chanya.

Kondo alisema wamepanga kurejea nyumbani wakiwa na kikombe cha mashindano hayo na wao watacheza kila mechi sawa na fainali.

"Tunatarajia kuonyesha soka la ushindani, tunawaheshimu wapinzani wetu wote, tunafahamu wazi hakuna mechi rahisi katika mashindano haya, kila timu imejiandaa na imejipanga kusaka matokeo bora, hivyo tunatarajia kukutana na ushindani katika kila mechi," alisema Kondo.

Kocha huyo aliongeza kikosi chake kimefanya mazoezi kwa muda mrefu pamoja na kucheza mechi mbalimbali za kirafiki, hivyo wachezaji wake wako tayari kupeperusha vyema bendera ya Tanzania Bara.

Tanzania Bara itaanza kusaka ubingwa wa michuano hiyo kesho kwa kuwakaribisha Uganda halafu itashuka tena dimbani Novemba 29, mwaka huu kuwakabili Sudan Kusini na itamaliza hatua ya makundi Desemba Mosi, mwaka huu kwa kuwavaa Zanzibar.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa CECAFA, Auka Gecheo, aliliambia gazeti hili maandalizi yote yamekamilika na wanatarajia kuona wachezaji wakionyesha ushindani katika kila mechi watakayocheza.

Gecheo (pichani) alisema anaamini mashindano hayo ni sehemu nyingine muhimu ya kuwaandaa wachezaji wa ukanda huu na michuano mbalimbali ya kimataifa iliyoko mbele yao.



## ZISIKUPITE

### MBAPPE KUIKAMUA MADRID

REAL Madrid iko tayari kutumia fedha msimu ujao baada ya kuelekeza macho yao kwa mshambuliaji wa Paris St-Germain na Ufaransa, Kylian Mbappe, mwenye umri wa miaka 24, na mshambuliaji wa Manchester City na Norway, Erling Haaland (23). ***(AS)***

### MAATSEN AKARIBIA CITY

MLINZI wa kushoto wa Chelsea, Ian Maatsen, mwenye umri wa miaka 21 yuko tayari kujiunga na Manchester City baada ya washindi hao wa mataji matatu kuhusishwa na kutaka kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi ya U-21. ***(Football Insider)***

### RAYA KUSAJILIWA ARSENAL

ARSENAL imekubali kufikia kipengele cha kumnunua mlinda mlango wa Brentford, David Raya, mwenye umri wa miaka 28, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania akitarajiwa kuwa mchezaji wa kudumu Januari kwa pauni milioni 27. ***(Fabrizio Romano)***

### NETO AGOMBEWA SOKONI

KLABU za Manchester United, Arsenal na za Saudi Arabia zinavutiwa na winga wa Timu ya Taifa ya Ureno, Pedro Neto mwenye umri wa miaka 23, lakini Wolves watataka ada ya angalau pauni milioni 60. ***(TeamTalks)***

### TODIBO ANUKIA UNITED

KLABU ya Manchester United inataka kuongeza nguvu katika safu ya beki wa kati, huku mlinzi wa Nice ya Ufaransa, Jean-Clair Todibo, 23, na mlinzi wa Sporting Lisbon wa Ureno, Goncalo Inacio (22), wakionekana kuwa bora kuchukua nafasi ya mchezaji wa zamani wa Ufaransa, Raphael Varane (30). ***(Sun)***

### CASEMIRO NJIA MOJA

KIUNGO wa kati wa Brazil, Casemiro, 31, anaweza kuwa njiani kuondoka Manchester United ifikapo Januari huku Mashetani Wekundu hao wakipania kukirekebisha kikosi chao. ***(TeamTalks)***

### AIT-NOURI KUTUA CHELSEA

KLABU ya Wolves inakabiliwa na kibarua cha kumshikilia mlinzi mahiri, Rayan Ait-Nouri, baada ya Chelsea kumwongeza mchezaji huyo wa kimataifa wa Algeria mwenye umri wa miaka 22 kwenye orodha yao wanaowaniwa. ***(90min)***

### WILLIAN ANUKIA CHELSEA

CHELSEA inamfuatilia winga wa Palmeiras, raia wa Brazil, Estevao Willian, 16, ambaye anasemekana ana kipengele cha kuachiliwa cha pauni milioni 52. ***(Mundo Deportivo)***

### DIAO KUTUA ENGLAND

WINGA wa Real Betis, Assane Diao mwenye umri wa miaka 18 anaonekana kulengwa na Brentford na klabu hiyo ya Ligi Kuu England inaweza kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania chini ya umri wa miaka 21 Januari. ***(Sky Sports)***

### SANGANTE KUTUA EPL

KLABU ya Newcastle United na Wolves zinaweza kumgombea mlinzi wa Senegal, Arouna Sangante mwenye umri wa miaka 21, baada ya kuvutia kwenye Ligue 1 akiwa na Le Havre. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND KAMILI KUIVAA LIVERPOOL

**MANCHESTER,** England

●●● Ni katika mechi ya Ligi Kuu England itakayochezwa leo baada...

ERLING Haaland yuko fiti kuitumikia Manchester City katika mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya Liverpool utakaochezwa leo baada ya kurejea mazoezini kutoka jeraha alilolipata kwenye majukumu ya kimataifa, kwa mujibu wa ESPN.

Haaland, ambaye anaongoza kwa orodha ya wafungaji mabao (13) kwenye Ligi Kuu England, aliumia kifundo cha mguu wakati wa ushindi kwenye mchezo wa kirafiki wa kimataifa wakati Norway ilipoikabili Visiwa vya Faroe Alhamisi iliyopita.

Maumivu aliyopata yalimfanya alazimike kujiondoa kwenye kikosi kilichocheza mechi ya kufuzu euro 2024 dhidi ya Scotland.

**Daktari wa timu ya Norway alisema Haaland alikuwa na "maumivu makubwa" na jeraha hilo, ambalo lilizidisha shida kama hiyo aliyoipata wakati wa akicheza dhidi ya Bournemouth mapema msimu huu.**

Lakini baada ya kurejea Manchester City kwa matibabu mwanzoni mwa wiki hii, Haaland alirejea mazoezini Alhamisi na kumpa uhakika Kocha, Pep Guardiola, kabla ya kukutana na Liverpool walio katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Ukrasa wa X (zamani Twitter) wa Manchester City jana uliweka picha ya Haaland mwenye umri wa miaka 23 akiwa mazoezini kwenye uwanja wa mazoezi wa klabu hiyo na alionekana kuwa na utimamu wake.

Guardiola jana alitarajiwa kutoa taarifa kuhusu kupona kwa Haaland wakati alipofanya mkutano wake na waandishi wa habari.

# MOURINHO: ANCELOTTI USIONDOKE MADRID



**ROME,** Italia

KOCHA wa Roma, Jose Mourinho, amemshauri Carlo Ancelotti kutoondoka Real Madrid, akisema Mtaliano huyo atakuwa "mwendawazimu" kuacha jukumu hilo kwenye mji mkuu wa Hispania na kwenda kuinoa Timu ya Taifa ya Brazil.

Rais wa Shirikisho la Soka la Brazil (CBF), alidai mnamo Julai, Ancelotti ataifundisha timu ya taifa ya nchi hiyo katika michuano ya Copa America 2024 itakayofanyika Marekani, ingawa hakuna mkataba kati ya pande hizo mbili ambao umesainiwa.

Katika mahojiano na kituo cha TG1 cha Italia, Mourinho alisema: "Nadhani ni mwendawazimu pekee ndiye anaweza kuondoka Real Madrid wakati bado anahitajiwa.

"Nina hakika katika ishara ya kwanza kutoka kwa Florentino (Perez, Rais wa Madrid), Carlo atabaki, kwa sababu ni kamili kwa Real Madrid na Real Madrid ni kamili kwake."

Bosi huyo wa Roma pia alisema yeye ndiye pekee "mwendawazimu" aliyeacha nafasi hiyo kule Madrid licha ya kuungwa mkono na Perez, na akasisitiza nia yake ya kufundisha Saudi Arabia wakati fulani huku kukiwa na sintofahamu kuhusu mustakabali wake ndani ya Roma.

Mkataba wake katika klabu hiyo ya Serie A unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

"Nitabaki Roma? Sijui," alisema Mourinho, akibainisha mazungumzo yake ya hivi karibuni na mmiliki wa Roma, Dan Friedkin hayakufikia mwafaka.

"Kusema ukweli, nadhani siku moja nitakwenda Saudi Arabia," alisema kocha huyo raia wa Ureno.

"Lakini ninaposema 'siku moja,' simaanishi leo au kesho."

Oktoba mwaka huu Mourinho alikiambia kituo cha televisheni cha MBC Misri, ambacho kinamilikiwa na kundi la Saudi la MBC, "nina Imani nitafundisha katika taifa hilo la Ghuba wakati fulani."

## Wan-Bissaka atakiwa DR Congo

**MANCHESTER,** England

BEKI wa Manchester United, Aaron Wan-Bissaka amepokea mwaliko wa kuiwakilisha Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) katika ngazi ya kimataifa, kwa mujibu wa 90min.


Licha ya wakati fulani katika maisha yake ya soka kuzingatiwa beki bora wa kulia kwenye Ligi Kuu England na United wakakubali kutoa pauni milioni 50 kumchukua kutoka Crystal Palace mwaka 2019, Wan-Bissaka anabakia ndio mchezaji ghali zaidi duniani ambaye hajaichezea timu ya taifa ya wakubwa.

Nafasi hiyo kuna wakati ilikuwa inashikiliwa na beki wa kulia Chelsea, Wesley Fofana lakini aliichezea Ufaransa kwa dakika 90 dhidi ya Gilbraltar mnamo Juni, mwaka huu.

Marc Cucurella (pauni milioni 62) aliichezea Hispania mara moja mwaka 2021 na Romeo Lavia (pauni milioni 58) aliitumikia Ubelgiji mechi ya kwanza mapema mwaka huu sasa amebakia Wan-Bissaka.

Wan-Bissaka ambaye ni mzaliwa wa Croydon aliiwakilisha England katika timu za vijana chini ya umri wa miaka 20 na 21 na aliitwa na kocha Gareth Southgate wakati wa mapumziko ya kwanza ya kimataifa ya msimu wa 2019/20, lakini alijiondoa kikosini baada ya kuumia.





# Alves hatarini kufungwa jela

**BARCELONA,** Hispania

WAENDESHA mashtaka wa Serikali ya Hispania wataomba kifungo cha miaka tisa jela kwa beki wa Brazil, Dani Alves, nyaraka za mahakama zinaonyesha, kwa mujibu wa ESPN.

Alves mweye umri wa miaka 40 atakabiliwa na tuhuma za kumnyanyasa kingono mwanamke katika klabu moja ya usiku iliyotokea Desemba, mwaka 2022.

Ofisi ya waendesha mashtaka pia itadai euro 150,000 kama fidia kwa mshtakiwa huyo anayedaiwa. Tarehe ya kesi bado haijapangwa.

Katika amri, Kifungu cha 21 cha Mahakama Kuu ya Barcelona hivi karibuni kilithibitisha kushtakiwa kwa Alves, na kuhitimisha maelezo ya mtuhumiwa na mashahidi, pamoja na uthibitisho wa kitaalamu, yanatoa ushahidi wa kutosha kumshtaki kwa uhalifu wa unyanyasaji wa kijinsia.

Mchezaji huyo wa zamani wa Barcelona na Paris Saint-Germain alizuiliwa Januari baada ya kushtakiwa kwa kumbaka msichana mdogo katika bafu la klabu ya usiku huko Barcelona Desemba 30, 2022.

Alves tangu wakati huo amekuwa kizuizini bila dhamana katika gereza la Barcelona, na maombi yake ya kuachiwa yamegonga mwamba mara kwa mara, kwa sababu anachukuliwa anaweza kukimbia.

Madai hayo yalipoibuka mara ya kwanza, Alves alikanusha katika mahojiano ya runinga kuwa hamfahamu mwanamke huyo.

Baadaye alisema alifanya mapenzi na mshtaki kwa makubaliano.

Mkataba wa Alves na klabu ya Liga MX Pumas UNAM, ambayo alijiunga nayo baada ya kuondoka Barcelona Juni, mwaka 2022 ulikatizwa Januari 20, mwaka huu.

Kesi ya ubakaji nchini Hispania adhabu yake ya juu ni kifungo cha miaka 15 jela.

# KMKM yajipanga kuimaliza Mafunzo

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

RAUNDI ya 12 ya Ligi Kuu Zanzibar inatarajiwa kuendelea leo kwa mabingwa watetezi, KMKM kuivaa Mafunzo kwenye Uwanja wa Mau A huku Uhamiaji FC ikiwakaribisha Maendeleo kutoka Kisiwani Pemba kwenye Uwanja wa Mau B.

Hata hivyo, KMKM itakuwa na kibarua kizito katika mechi ya leo kutokana na kutofanya vizuri tangu kuanza kwa msimu huu ikilinganishwa na makali yake ya misimu iliyopita.

Katika michezo 11 iliyocheza, KMKM imeshinda michezo mitano, sare michezo miwili na imefungwa michezo minne.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Msaidizi wa KMKM, Ame Msimu, alikiri Ligi Kuu Zanzibar msimu huu imekuwa ngumu kutokana na kila timu kujiandaa vyema.

Msimu alisema hawajaanza vyema mzunguko wa kwanza na wanatarajia kufanya tathmini ili kupata matokeo bora katika michezo inayofuata.

Alisema tatizo kubwa katika kikosi chake lilikuwa wachezaji wake wengi wa kikosi cha kwanza kuwa majeruhi hivyo kusababisha kutumia nyota ambao hawana uzoefu na ligi hiyo.

"Kutokana na ugumu wa ligi tumekuwa tukiongeza idadi ya majeruhi kila mechi, kuna wakati kama benchi tunakuwa na wakati mgumu katika kupanga kikosi hasa pale tunapokutana na vigogo wa ligi hii," alisema kocha huyo.

Aliongeza wanatarajia kupata ushindi katika mechi hiyo ingawa anajua wanakutana na timu iliyoko kwenye nafasi mbaya na inayohitaji pia kujinusuru.

**Kutokana na ugumu wa ligi tumekuwa tukiongeza idadi ya majeruhi kila mechi, kuna wakati kama benchi tunakuwa na wakati mgumu katika kupanga kikosi hasa pale tunapokutana na vigogo wa ligi hii.**

# MR & MISS DEAF WORLD 2023 KUFANYIKA DAR LEO

Na Saada Akida

SHINDANO la kusaka washindi wa taji la urembo kwa watu wenye ulemavu wa kusikia duniani (Mr and Miss Deaf World 2023) linatarajia yanayofanyika leo kwenye ukumbi wa Super Dom uliopo Masaki, Dar es Salaam.

**Hii ni mara ya pili kwa Tanzania kuwa mwenyeji wa mashindano hayo ya kimataifa.**

Akizungumza na Nipashe jijini jana, Mkurugenzi wa Idara ya Sanaa, Dk. Emmanuel Ishengoma, alisema Tanzania imepata uenyeji wa kuandaa mashindano hayo kutokana na kuonyesha nidhamu na kiwango bora katika fainali zilizofanyika mwaka jana.

Ishengoma alisema kupitia mashindano hayo nchi inapata nafasi ya kutangaza kimataifa pamoja na vivutio vyake mbalimbali vya utalii.

Alisema mashindano hayo yanashirikisha watu maalumu lakini pia yanatoa fursa kwa washiriki kujiendeleza kupitia nafasi mbalimbali watakazopata baada ya kumalizika kwa fainali hizo.

"Mwaka jana tulifanya vizuri na viongozi wameona pia mwaka huu Tanzania iwe mwenyeji kwa mara ya pili, mashindano haya ni ya makundi maalum, kupitia huu wenyeji tunapata fursa mbalimbali ikiwamo kutangaza utalii wa Tanzania kwa sababu yanajulikama dunia nzima, Tanzania tumetoa washiriki 10," alisema Ishengoma.

Naye mwalimu wa washiriki kutoka Tanzania, John Victor 'Mack', alisema anaamini wenyeji watafanya vyema katika mashindano hayo kutokana na maandalizi waliyofanya.

Mack alisema washiriki wa Tanzania wako vizuri na wameahidi kuzingatia maelekezo waliyopewa ili kufanya vyema katika shindano hilo.

"Mwaka huu tumejipanga vizuri, ninaimani na wawakilishi wetu, hawatatuangusha kwa sababu tumefanya maandalizi mazuri na kutumia bidhaa za hapa nyumbani ikiwamo ngoma za kiutamaduni," alisema Mack.



Katibu Msaidizi wa Idara ya Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Shaibu Akwilombe (kulia) akikabidhi ng'ombe watano kwa Mshauri wa Baraza la Wazee wa Yanga ikiwa ni ahadi iliyotolewa na Katibu wa Itikadi na Uenezi, Paul Makonda, kabla ya mechi ya watani wa jadi iliyomalizika kwa Yanga kupata ushindi wa mabao 5-1. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# *Simba: Tutawafuta machozi*

INATOKA UKURASA 24

mechi hiyo ya hatua ya makundi ambayo baadhi ya timu nyingine bora zimekosa nafasi hiyo.

"Tunauzoefu wa muda mrefu na ninaimani ya kufanya vizuri katika mchezo dhidi ya Simba, tutapambana kupata matokeo mazuri ikiwa ni mchezo wa kwanza hatua ya makundi," alisema Jullien.

Aliongeza timu hiyo ilipitia changamoto nyingi ikiwamo ya Covid 19 kwa kushindwa kushiriki vizuri mashindano ya kimataifa lakini sasa wako imara na wamekuja Tanzania kutafuta matokeo chanya.

Aliweka wazi ameifuatilia Simba kutumia mechi zake mbalimbali na si kupata taarifa kupitia wachezaji ambao waliichezea timu yake na sasa wako Yanga ili kuwafahamu wapinzani wao.

"Tunasahau matokeo ya mwisho na hayapo katika vichwa vyetu kwa sababu kwa sasa tunaangalia kilichoko mbele yetu ni kutafuta ushindi dhidi ya Simba," alisema Jullien.

Nahodha wa Asec Mimosas, Essie Aka, alisema wamejiandaa vizuri na hakuna cha ziada walichokuja nacho zaidi ya kucheza na Simba ili kupata matokeo chanya.

Aka alisema wameshiriki mashindano mengi na wamekutana na timu mbalimbali hivyo wamepata uzoefu na wanasubiri kuona dakika 90 zitakavyoongea.

# Aziz Ki aendelea 'kukimbiza'

INATOKA UKURASA 24

Martini Kigi wa JKT Tanzania, Cheikh Sibibe wa Azam FC, Valentino Mashaka wa Geita Gold, Dissan Galiwango wa Kagera Sugar, Edwin Barua wa Prisons, Marouf Tchakei na Gadiel Michael wa Singida Fountain Gate, na Omari Kindamba wa Mashujaa FC.

Wakati huo huo, kabla ya mechi za jana, jumla ya penalti 12 zimepatikana kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, huku 10 zikiwa zimewekwa wavuni.

Timu za Simba na Namungo zinaongoza kwa kufunga penalti nyingi mpaka sasa, kila mmoja ikiweka wavuni penalti mbili, Wekundu wa Msimbazi wakifunga kupitia Saido Ntibazonkiza na Baleke huku Fabrice Ngoyi na Derrick Mukombozi wakiifungia Namungo ya mkoani Lindi.

Wachezaji wengine waliofunga penalti moja kila mmoja ni, Erick Okutu wa Tabora United, Lucas Kikoti (Mtibwa Sugar), Obrey Chirwa (Kagera Sugar), Pacome Zouzoua ( Yanga) na Prince Dube wa Azam FC.

# Michezo

Jumamosi Novemba 25, 2023

Nipashe




Haaland kamili kuivaa Liverpool UKURASA 21



Nahodha wa Simba, John Bocco (kushoto) na beki wa timu hiyo, Mohammed Hussein wakifanya mazoezi kuelekea mechi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya ASEC Mimosas itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA SC**

## Aziz Ki aendelea 'kukimbiza' Ligi Tanzania Bara

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki, anaongoza kwa kufunga mabao ya faulo akiwa amefunga mabao mawili ya aina hiyo.

Aziz Ki ambaye mpaka sasa ni mmoja wa wanaoongoza katika orodha ya wafungaji bora akiwa na mabao saba, sawa na Maxi Nzengeli wa Yanga na Jean Baleke wa Simba, amepachika magoli mawili ya faulo huku wenzake wakiwa hawana hata bao moja la 'fri-kiki.'

Hakuna mchezaji yoyote katika Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa aliyefunga mabao mawili kwa njia hiyo, huku jumla ya mabao 11 yakiwa yamewekwa wavuni kwa adhabu ndogo.

Bao lake la kwanza la faulo alifunga Agosti 29, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Yanga ikiitandika JKT Tanzania mabao 5-0 na lingine alifunga Oktoba 23, mwaka huu Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam mabingwa hao watetezi wakiifunga Azam FC mabao 3-2.

Kwa mujibu wa dawati letu la takwimu, Yanga na Singida Fountain Gate, ndio zenye mabao mengi yaliyofungwa kwa faulo, kila moja ikipata mawili.

Wachezaji wengine tisa waliofunga mabao kwa 'fri-kiki', kila mmoja akifunga goli moja ni Ibrahim Ajibu wa Coastal Union,

ENDELEA UKURASA 23

# *Simba: Tutawafuta machozi*

## ●●● Kocha, wachezaji waahidi kandanda safi ikiwaalika Asec Mimosas katika...

**Na Saada Akida**

FURAHA ndio kitu pekee kilichoko katika vichwa vya wachezaji wa Simba kuelekea mechi ya Kundi B ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Asec Mimosas kutoka Ivory Coast itakayochezwa leo kuanzia saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Mara ya mwisho timu hizo zilikutana kwenye uwanja huo huo na Simba iliibuka na ushindi wa mabao 3-1, lakini ikiwa ni hatua ya makundi katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.**

Simba iliyoko katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kushinda mechi sita, sare moja na kufungwa mchezo mmoja inawaalika Asec Mimosas ambao wanaongoza katika Ligi Kuu ya Ivory Coast, wakishinda michezo saba, sare moja na wamepoteza mechi tatu.

Kuelekea mechi ya leo, Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Daniel Cadena, alisema wamefanyia kazi kila eneo ikiwamo kuwajenga kiakili, kimwili na kiufundi wachezaji wake na kuongeza kikosi kipo tayari kwa mchezo huo.

Cadena alisema katika mechi ya leo atakosa huduma ya nyota wake wawili ambao ni Clatous Chama, ambaye amechelewa kujiunga na timu akitokea kwenye majukumu ya kimataifa pamoja na kipa, Aishi Manula, aliyepata jeraha dogo katika mchezo uliopita kati ya Niger dhidi ya Taifa Stars.

"Hatukuwa na matokeo mazuri katika mechi iliyopita, tumepata muda wa kujiandaa na kubadilisha vitu vingi ninaimani tutapata matokeo mazuri kulingana na maandalizi tuliyofanya.

Asec Mimosas tumewaona na tutacheza kwa tahadhari kubwa ili kuhakikisha tunafanikiwa kutumia vizuri uwanja wa nyumbani kwa kuibuka na ushindi hapo kesho (leo)," alisema Cadena.

Kocha huyo amewataka mashabiki wa timu hiyo kujitokeza kwa wingi kwa sababu nguvu yao inasaidia kuongeza ushindani na kuwaambia watarajie kupata ushindi katika mchezo huo.

Mwakilishi wa wachezaji wa Simba, Che Malone Fondoh, alisema hawana cha kuahidi zaidi ya kusema wanakwenda kupambana kutafuta ushindi katika mchezo huo.

Che Malone alisema wanatarajia kurudi katika njia yao ya kupambana kutafuta matokeo mazuri kwa kucheza kwa kufuata maelekezo waliyopewa na benchi la ufundi ili kufikia malengo.

"Tumejiandaa vizuri, kikubwa mashabiki kujitokeza kwa wingi uwanjani kutusapoti, maandalizi yameenda vizuri na matarajio yetu ni kushinda katika mchezo wetu huu," alisema Che Malone.

Kocha Mkuu wa Asec Mimosas, Jullien Chevaller, alisema anafuraha ya kufika salama Tanzania kwa ajili ya kucheza

ENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >